Haliuzwi

JULAI 13, 2026

/islamicftz

Muharram 28 1448

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 592

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## SHEIKH HAMAD AL THANI
Ulimwengu wa Kiislamu wamlilia



# Maridhiano yaimarisha matumaini ya mshikamano, maendeleo Zanzibar

## Samia: Wanaojiita wanaharakati wanafanya ugaidi


"Niwaonye kwa mara nyingine wote wanaojishughulisha na vitendo hivyo, kwamba Taifa lolote duniani hutumia vyombo vya dola kuhami wananchi wake na kulinda heshima yake. Nasi Tanzania kama Taifa hatutasita kufanya hivyo."





## Mwinyi: Misikiti isiishie ibada, iwe shule ya maadili

## Walimu wa EDK wanapochukuliwa kama watumishi daraja la tatu



## Madhila yanayowakumba watoto duniani



## Srebrenica yaendelea kuzika waathirika wa mauaji ya kimbari



إنا لله وإنا إليه راجعون


## Sheikh Hamad Al Thani

# Ulimwengu wa Kiislamu wamlilia

محرم

إِنَّا لِلَّٰهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

## SHEIKH HAMAD AL THANI



# Ulimwengu wa Kiislamu wamlilia

***DOHA, Qatar,*** Aliyekuwa Amir wa Qatar, Sheikh Hamad bin Khalifa Al Thani, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 74, akiacha urithi mkubwa wa maendeleo, uongozi na kuimarisha nafasi ya Qatar katika ulimwengu wa Kiarabu na Kiislamu.

Serikali ya Qatar ilitangaza kifo chake Jumapili, ikisema taifa limepata msiba mkubwa. Ofisi ya Amir ilisema imeupokea msiba huo kwa imani katika hukumu na makadirio ya Mwenyezi Mungu, huku ikiomba marehemu arehemewe.

Sheikh Hamad aliiongoza Qatar kwa miaka 18, kuanzia mwaka 1995 hadi 2013, alipomkabidhi madaraka mwanawe, Amir Sheikh Tamim bin Hamad Al Thani.

Alivyoibadilisha Qatar kiuchumi

Katika kipindi chake, Qatar ilibadilika kutoka taifa lenye uchumi mdogo uliotegemea zaidi mafuta na kuwa moja ya nchi tajiri na zenye ushawishi mkubwa duniani.

Msingi mkubwa wa mageuzi hayo ulikuwa uendelezaji wa hazina ya gesi ya North Field, ambayo ni miongoni mwa maeneo makubwa zaidi ya gesi duniani.

Qatar ilisafirisha shehena yake ya kwanza ya gesi asilia iliyosindikwa kuwa kimiminika (LNG) mwaka 1996 na ndani ya kipindi kisichozidi miaka 15 ikawa msafirishaji mkubwa zaidi wa bidhaa hiyo duniani.

Kufikia mwaka 2010, uwezo wa uzalishaji wa LNG ulikuwa umefikia tani milioni 77 kwa mwaka, hatua iliyoiweka Qatar katika nafasi muhimu katika usalama wa nishati duniani.

Ukuaji huo uliibadilisha pia hali ya uchumi. Pato la taifa liliongezeka kutoka karibu dola bilioni nane mwaka 1995 hadi takribani dola bilioni 199 mwaka 2013.

Sheikh Hamad alitumia mapato ya nishati kujenga taasisi, miundombinu na vitega uchumi vya muda mrefu. Serikali yake ilianzisha Baraza Kuu la Masuala ya Uchumi na Uwekezaji pamoja na Mamlaka ya Uwekezaji ya Qatar.

Kupitia taasisi hizo, Qatar iliwekeza katika kampuni, benki, majengo na miradi mikubwa duniani. Mkakati huo ulilenga kulinda utajiri wa taifa na kuandaa vyanzo vya mapato kwa vizazi vijavyo.

## Elimu, afya na miundombinu

Ndani ya Qatar, mapato hayo yalielekezwa katika elimu, afya, nyumba, usafiri na miundombinu. Miradi kama Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Hamad, Bandari ya Hamad, mji wa Lusail na barabara za kisasa ilibadili sura ya Doha.

Mwaka 1995, Qatar Foundation for Education, Science and Community Development ilianzishwa kwa lengo la kuimarisha elimu, utafiti na ubunifu.

Baadaye, vyuo vikuu maarufu duniani vilifungua matawi na programu nchini Qatar, hatua iliyosaidia kujenga uchumi unaotegemea maarifa pamoja na rasilimali za asili.

Mageuzi hayo yalisaidia pia kuinua huduma za afya, makazi na ustawi wa wananchi, huku Qatar ikifikia miongoni mwa viwango vya juu vya mapato kwa kila mtu duniani.

## Msaada wake kwa Palestina

Hamas imemuelezea Sheikh Hamad kuwa kiongozi mkubwa wa kitaifa na Kiarabu aliyesimama pamoja na watu wa Palestina na kuunga mkono haki yao ya uhuru.

Kundi hilo limesema marehemu alifanya ustawi wa taifa lake, wananchi wake na Umma wa Kiislamu kuwa sehemu ya msingi ya uongozi wake.






NA ABUU IPTISAM,
KILOSA, MOROGORO

# Maridhiano yaimarisha matumaini ya mshikamano, maendeleo Z'bar

Hatua ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT-Wazalendo kusaini tamko la pamoja la maridhiano imeendelea kuimarisha matumaini ya umoja, maelewano na amani Zanzibar, baada ya miezi kadhaa ya mazungumzo yaliyolenga kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizojitokeza baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Makubaliano hayo, yaliyotiwa saini Julai 9, 2026, yanaweka msingi wa kuendelezwa kwa mazungumzo na utekelezaji wa hatua mbalimbali zinazolenga kuimarisha mshikamano wa wananchi, utawala bora na maendeleo ya Zanzibar.

Tamko hilo lilifikiwa baada ya mazungumzo yaliyoanza Novemba 2025, chini ya uongozi wa marais wastaafu wa Zanzibar, Dkt. Amani Abeid Karume na Dkt. Ali Mohamed Shein.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, pande hizo zimekubaliana kuunda kamati ya pamoja itakayopanga mfumo, utaratibu na upeo wa utekelezaji wa ajenda zilizokubaliwa. Baadaye, chombo maalumu cha kisheria kitaundwa kwa ajili ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa maamuzi hayo.

Miongoni mwa maeneo yatakayofanyiwa kazi ni marekebisho ya Katiba ya Zanzibar, mfumo wa uchaguzi, utumishi wa umma, mfumo wa haki, utawala wa serikali za mitaa na hatua za kuimarisha imani ya wananchi katika taasisi za umma.

Makubaliano hayo pia yanalenga kuweka mazingira ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, pamoja na kuendeleza misingi ya uwajibikaji, utawala wa sheria na ushiriki mpana wa wananchi katika maendeleo.

Kwa jamii ya Zanzibar yenye Waislamu wengi, maridhiano hayo yana umuhimu mkubwa zaidi ya tofauti za kisiasa. Uislamu unahimiza suluhu, kusameheana, kuheshimiana na kuepusha mifarakano inayoweza kuvunja undugu na kuhatarisha usalama wa jamii.

Siku moja baada ya kutiwa saini kwa tamko hilo, Rais wa Zanzibar, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, alitumia jukwaa la Sala ya Ijumaa na ufunguzi wa Msikiti wa Abrar, Fuoni Kibondeni, kusisitiza kuwa dhamira ya maridhiano ni kuwaunganisha wananchi na kuwawezesha kushirikiana katika kuleta maendeleo.

Aliwataka wananchi kusahau yaliyopita, kusameheana, kuachana na mifarakano na kusonga mbele kwa pamoja. Alisema umoja, mshikamano, amani na maelewano ndiyo misingi inayoiwezesha Serikali kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kauli hiyo inaipa jamii nafasi muhimu katika kuendeleza maridhiano. Viongozi wa dini, maimamu, walimu wa madrasa, wazazi na vijana wanaweza kusaidia kuimarisha lugha ya staha, kuvumiliana na kujenga utamaduni wa kusikilizana.

Rais Mwinyi pia alihimiza misikiti kutumika kama sehemu za ibada, malezi na majadiliano ya changamoto za jamii. Kwa nafasi hiyo, misikiti inaweza kuwa majukwaa muhimu ya kuimarisha msamaha, kusuluhisha tofauti na kujenga kizazi kinachotanguliza maslahi ya jamii.

Maridhiano hayo yanafungua ukurasa mpya wa ushirikiano Zanzibar na kutoa fursa ya wananchi kuelekeza nguvu zao katika elimu, biashara, huduma za jamii, malezi ya vijana na maendeleo ya familia kwa mazingira ya amani na utulivu.



Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi akipeana mkono na Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman baada ya kushuhudia utiaji saini wa ajenda zilizokubaliwa na pande mbili kwa ajili ya kufanyiwa kazi kufuatia tamko la pamoja la mwafaka wa kisiasa baina ya CCM na ACT-Wazalendo, katika hafla iliyofanyika viwanja vya Ikulu Zanzibar. Picha na Ikulu

NA MWANDISHI WETU

# Rais Samia asema wanaojiita wanaharakati wanafanya ugaidi

Rais Samia Suluhu Hassan amewaonya watu wanaojiita 'wanaharakati' akiyaita matendo yao kuwa ya kigaidi huku akisema Serikali haitasita kutumia vyombo vya dola kuhami wananchi wake na kulinda heshima ya nchi.

Rais Samia alisema hayo jana mjini Unguja, Zanzibar wakati akishuhudia hafla ya utiaji saini wa tamko la pamoja la maridhiano ya kisiasa baina ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na ACT- Wazalendo.

Alitumia nafasi hiyo kuwaonya wale aliosema wanaojiita wanaharakati kwa jina ili watambulike duniani, lakini kiuhalisia matendo yao ni ya kigaidi.

Alifafanua kuwa, ugaidi unajumuisha vitendo vya uvunjifu mkubwa wa amani, uharibifu wa mali na miundombinu, vinavyokusudia kuitishia jamii au kuishurutisha Serikali kukubaliana na matakwa ya watu au kundi fulani kwa ajili ya kutimiza haja za kisiasa, kiitikadi au kidini.

Kwa mustakabali wa dunia ya sasa, ugaidi unaweza kutumika kuirudisha nyuma nchi inayoendelea kwa kasi. Watu au kundi hilo, wanakuwa na kauli zinazovaa sura ya kizalendo lakini kwa undani ni masilahi binafsi.

"Mtu anayeipenda nchi yake, kiukweli, huijenga na siyo kuibomoa. Upande huu tumeipenda nchi yetu, tumetofautiana, tumevumiliana, hatukufanya vurugu za kubomoa nchi yetu wala uvunjifu wa amani.

"Nawasihi Watanzania, tushikamane kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu na siyo kulifanya Taifa kuwa duni kwa matakwa ya watu binafsi ambao maisha yao huko waliko na hata hapa nchini, yanategemea malipo yatokanayo na kufanya vurugu au kuivuruga nchi yao kwa maslahi ya wengine," alisema Rais Samia.

Mkuu huyo wa nchi aliwahakikishia Watanzania kwamba, Serikali itasimama imara katika ulinzi wa raia wake na mali zao, pia, aliwataka wananchi kuungana na Serikali kulinda maeneo yao na mali zao.

"Vitendo vya kigaidi katu havikubaliki, siyo kwa Tanzania tu, bali ulimwengu mzima. Hivyo basi, niwaonye kwa mara nyingine wote wanaojishughulisha na vitendo hivyo, kwamba Taifa lolote duniani hutumia vyombo vya dola kuhami wananchi wake na kulinda heshima yake. Nasi Tanzania kama Taifa hatutasita kufanya hivyo," alisisitiza.

Aliongeza kuwa, Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi zote zenye dhamira ya kulinda amani, kuendeleza umoja wa muungano na kuimarisha ustawi wa wananchi. Alisema Zanzibar ikiwa na amani, Tanzania inakuwa salama.

"Amani ni mtaji, maridhiano ni daraja na wananchi ndiyo sababu ya uongozi wetu, hatuna budi kuwatumikia kwa amani na utulivu," alisema Rais Samia.

## Maridhiano si udhaifu

Rais Samia alisema maridhiano si udhaifu bali ni ukomavu wa kisiasa unaojenga misingi ya umoja na kuheshimiana.

Alisema ni ishara kwamba viongozi wanaweza kutofautiana lakini wakakubaliana katika mambo ya msingi ya uendeshaji wa nchi, kujali masilahi ya wananchi na nchi kwa jumla.

"Mwelekeo huu wa kiungwana tulioshuhudia leo unafungua ukurasa mwingine katika kuimarisha umoja, amani, mshikamano na utulivu wa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla, jitihada hizi zinapaswa kuendelezwa na kuenziwa," alisema.

Alisema uungwana unatufunza kuwa na siasa za kushindana kwa hekima na si kupaza sauti bila mantiki, unafundisha siasa zinazotanguliza masilahi ya nchi na wananchi wake na siasa zinazotawaliwa na sauti zenye staha, utu, heshima na utulivu ili kufikia mustakabali wa pamoja wa kitaifa.

"Uungwana hautufunzi kiburi na kutosikilizana. Wananchi wetu hawahitaji vurugu wala mivutano ya kisiasa isiyoisha, wananchi wetu wanahitaji amani, usalama na utulivu. Shauku ya wananchi wote, bila kujali vyama vyao, ni kuona Serikali ikiwapa huduma bora za kijamii, ikiimarisha shughuli zao za kiuchumi na kukuza ajira katika mazingira yenye ustawi," alisema.

Alisema penye siasa za chuki, baraka za maendeleo hutoweka, lakini penye siasa za staha na maelewano, maendeleo hupata nafasi na kuchanua.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi pamoja na wageni mbalimbali waliohudhuria hafla ya uwasilishaji wa tamko la pamoja la mwafaka wa kisiasa baina ya CCM na ACT-Wazalendo katika viwanja vya Ikulu Zanzibar. Picha na Ikulu

NA MWANDISHI WETU

# Mwinyi: Misikiti isiishie ibada, iwe shule ya maadili





Misikiti imeelezwa kuwa nguzo muhimu ya kujenga jamii yenye hofu ya Mungu, maadili mema na mshikamano, huku ikitakiwa kuendelea kutumika si tu kama sehemu za ibada bali pia vituo vya malezi ya vijana, utoaji wa elimu na mapambano dhidi ya changamoto mbalimbali za kijamii.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema misikiti ina nafasi kubwa katika kuimarisha maadili ya jamii na kuhimiza amani, umoja na mshikamano unaohitajika ili kuharakisha maendeleo ya Zanzibar.

Akizungumza baada ya kushiriki Sala ya Ijumaa na kufungua Msikiti wa Abrar uliopo Fuoni Kibondeni, Mkoa wa Mjini Magharibi, Dkt. Mwinyi alisema taasisi za dini zina mchango mkubwa katika kujenga kizazi chenye maadili na kuwalea wananchi wanaoheshimu utu, sheria na misingi ya mshikamano wa kitaifa.

Alisisitiza kuwa misikiti inapaswa kutumika kama vituo vya ibada, malezi ya maadili na utoaji wa elimu inayosaidia kukabiliana na changamoto zinazoikabili jamii, ikiwemo mmomonyoko wa maadili, migogoro ya kifamilia na tabia zinazohatarisha ustawi wa vijana.

Rais Dkt. Mwinyi alisema Serikali itaendelea kuthamini mchango wa taasisi za dini katika kuimarisha maadili na kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika juhudi za maendeleo ya taifa.

Akizungumzia mchakato wa maridhiano ya kitaifa, Rais alisema dhamira yake ni kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar, kuimarisha umoja na mshikamano na kuweka mazingira bora yatakayowezesha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Aliwahimiza wananchi kusameheana, kuachana na tofauti zinazoweza kusababisha migawanyiko na kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali zinazolenga kuijenga Zanzibar yenye amani, utulivu na ustawi kwa wote.

Aidha, aliwataka wananchi kuendeleza utamaduni wa kusaidiana kwa kuwajali mayatima, wajane, watu wenye ulemavu na makundi mengine yenye mahitaji maalumu, akieleza kuwa mshikamano wa kijamii ni msingi muhimu wa maendeleo endelevu.

Katika hafla hiyo, Rais Dkt. Mwinyi alipongeza Taasisi ya Al Hilal Islamic Center kwa kufanikisha ujenzi wa Msikiti wa Abrar, akisema uwekezaji katika nyumba za ibada unaimarisha huduma za kiroho na kuchangia ustawi wa jamii kwa ujumla.

Baada ya shughuli hiyo, Rais Dkt. Mwinyi alitembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mjini Magharibi Lumumba, ambako alimjulia hali Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Magharibi Kichama, Ndg. Muhammed Rajab Soud, anayepatiwa matibabu hospitalini hapo.




HABARI ZANZIBAR

NA MWANDISHI WETU

# Rais Mwinyi aongoza maelfu kumzika mwanazuoni Z'bar

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ameungana na viongozi wa dini, serikali na wananchi katika mazishi ya mwanazuoni aliyeheshimika visiwani humo Sheikh Sayyid Othman bin Sayyid Abdulqadir Al Qadiry.

Rais Mwinyi alikuwa miongoni mwa waumini walioshiriki Swala ya Jeneza na baadaye maziko hayo yaliyohudhuriwa na wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi.

Mwanazuoni huyo alizikwa Alhamisi ya Julai 9, 2026 katika kijiji alichozaliwa cha Tunduni Mchangani, Mkoa wa Kaskazini Unguja, baada ya Swala ya Jeneza iliyosaliwa katika Msikiti wa Ijumaa wa Tunduni ikihudhuriwa na maelfu ya Waislamu waliojitokeza kumuombea msamaha kwa Mola wake.

Mapema, umati mkubwa wa waumini ulikusanyika katika Msikiti wa Ngamia (Baladul Amin) kwa ajili ya maandalizi ya awali ambako baada ya kuswaliwa na maelfu ya watu, maiti ya Sheikh Othman ilisafirishwa kutokea hapo kuelekea Tunduni.

Kutokana na wingi wa watu waliotaka kushiriki, magari mbalimbali ya kukodiwa ya abiria pamoja na ya vikosi vya majeshi, ikiwemo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), yalitumika kubeba na kusafirisha maelfu ya waombolezaji hao kuelekea kijijini kwao.

Sheikh Sayyid Othman alifariki dunia Julai 7, 2026 akiwa na umri wa miaka 88. Marehemu ameacha wajane watatu na watoto 11. Watu wengi waliohojiwa kuhusu namna walivyomjua marehemu, walimtaja kama mtu mpole, mkimya, mkarimu, aliyefanya kazi kubwa ya kulea yatima, kusomesha watu na kuanzisha madrasa na ujenzi wa misikiti.

Siku aliyofariki, aliamka asubuhi na kusali jamaa msikitini na kufanya adhkar hadi Jua liliochomoza aliosali sala ya Ishraq. Aliporejea nyumbani, baada ya kupata kifungua kinywa, alijisikia vibaya na umauti ukamfika.

Sheikh Othman alizaliwa mwaka 1938 katika kijiji cha Tunduni Mchangani na alitumia sehemu kubwa ya maisha yake kufundisha dini, kulea wafuasi na kusimamia shughuli za dini nchi nzima na Tanzania.

Rais Mwinyi amekiri kuwa kifo cha kiongozi huyo kimeacha pengo kubwa katika uongozi wa kiroho na elimu ya dini nchini, akitambuliwa kama kama mlezi, mwalimu na kiongozi kwa wengi waliomfuata awaongoze katika harakati za dini.

Tukio hili kubwa la majonzi limejiri katika siku ya kihistoria visiwani Zanzibar, ambapo vyama vikuu vya kisiasa vya CCM na ACT-Wazalendo vilisaini makubaliano mapya ya ushirikiano wa kisiasa nchini. Licha ya ratiba hiyo ngumu ya kiserikali na kisiasa, Rais Mwinyi alifika kuungana na wananchi kutoa heshima za mwisho kwa kiongozi huyo wa kiroho.



NA MWANDISHI WETU

# Visa vya Biriat, Hamis vyagusa wengi matokeo kidato cha 6



Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita mwaka 2026 yameonesha mafanikio ya baadhi ya shule za Kiislamu nchini, huku shule kadhaa zikipata ufaulu wa asilimia 100 na idadi kubwa ya watahiniwa wao wakipata Daraja la Kwanza na la Pili.

Pamoja na mafanikio ya shule hizo, matokeo hayo yameibua simulizi za wanafunzi wawili—Biriat Yafet Biriat, anayedaiwa kuongoza kitaifa, na Hamis Nguku, mwanafunzi mwenye ulemavu wa mikono anayeandika kwa kutumia miguu—ambazo zimeonesha thamani ya juhudi, malezi na msaada wa jamii katika elimu.

Uchambuzi wa matokeo ya Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) unaonesha kuwa Shamsiye Boys' Secondary School ilikuwa na watahiniwa 46, ambapo 42 walipata Daraja la Kwanza na wanne Daraja la Pili.

Istiqaama Tanga Islamic Secondary School nayo ilikuwa na watahiniwa 96 waliofaulu, wakiwamo 73 waliopata Daraja la Kwanza, 20 Daraja la Pili na watatu Daraja la Tatu.

Kirinjiko Islamic Seminary imeongeza orodha ya shule za Kiislamu zilizofanya vizuri. Kati ya watahiniwa wake 38, wanafunzi 18 walipata Daraja la Kwanza, 14 Daraja la Pili na sita Daraja la Tatu. Hakuna aliyepata Daraja la Nne wala kufeli.

Matangini Islamic Seminary ilikuwa na watahiniwa 16, ambapo 12 walipata Daraja la Kwanza na wanne Daraja la Pili. Ilala Islamic Secondary School nayo ilikuwa na watahiniwa 50, kati yao 33 wakipata Daraja la Kwanza, 16 Daraja la Pili na mmoja Daraja la Tatu.

Katika shule za wasichana, Uchira Girls' Islamic Secondary School ilikuwa na watahiniwa 30, ambapo 13 walipata Daraja la Kwanza na 17 Daraja la Pili. Al-Kheir Islamic Girls' Seminary nayo ilikuwa na watahiniwa 31; tisa wakipata Daraja la Kwanza, 17 Daraja la Pili na watano Daraja la Tatu.

Pemba Islamic College ilikuwa na watahiniwa 77 waliofaulu, wakiwamo 39 wa Daraja la Kwanza, 27 Daraja la Pili na 11 Daraja la Tatu.

Matokeo hayo yanaonesha kuwa jambo kubwa lililojitokeza katika shule nyingi za Kiislamu zilizochunguzwa ni kutokuwapo kwa watahiniwa waliopata Daraja la Nne au sifuri. Pia, shule hizo zimeonesha uwezo katika tahasusi za sanaa, biashara na sayansi sambamba na masomo ya dini.

Nje ya kundi hilo, Ndanda Secondary School imejitokeza kwa matokeo makubwa, ikiwa na watahiniwa 524 waliopata Daraja la Kwanza, 26 Daraja la Pili na mmoja Daraja la Tatu.

Miongoni mwa wahitimu wake ni Biriat Yafet Biriat kutoka Tunduru, ambaye ameripotiwa kuwa kinara wa kitaifa katika matokeo hayo. Mafanikio yake yalimfanya Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Ado Shaibu Ado, kukutana naye na kumpatia Sh milioni moja pamoja na simu, huku akiahidi kumnunulia kompyuta mpakato na kumsaidia katika hatua za kujiunga na elimu ya juu.

Biriat amesema msaada huo umemfungulia milango na unaweza kuwahamasisha wadau wengine kusaidia safari yake ya elimu.

Simulizi nyingine iliyogusa wengi ni ya Hamis Nguku, mwanafunzi wa Kilosa Secondary School mwenye ulemavu wa mikono ambaye huandika na kufanya shughuli nyingi kwa kutumia miguu.

Hamis alipata Daraja la Kwanza la pointi tano katika masomo ya sanaa. Kilosa Secondary School ilikuwa na watahiniwa 98, ambapo 89 walipata Daraja la Kwanza na tisa Daraja la Pili.


Mwalimu Mariam Msemakweli amesema Hamis alikuwa mmoja wa wanafunzi wawili tu shuleni hapo waliopata Daraja la Kwanza la pointi tano. Mafanikio yake yamekuwa ujumbe kwa wazazi kwamba watoto wenye mahitaji maalumu wanaweza kufanya vizuri wakipewa nafasi, vifaa na msaada unaofaa.

Hamis, aliyesaidiwa kielimu na Kalam Education Foundation, amewashukuru walimu na wanafunzi wenzake kwa kumsaidia katika shughuli ambazo hawezi kuzifanya kwa miguu.

Kwa ujumla, matokeo hayo yanaonesha kuwa uwekezaji katika nidhamu, walimu, mazingira ya kujifunzia na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji tofauti unaweza kuleta mafanikio makubwa. Kwa taasisi za Kiislamu, matokeo hayo yanatoa msingi wa kuendelea kuimarisha elimu ya dini sambamba na taaluma za kisasa.

Na Abeid Othman
0754 990 083

# Walimu wa EDK wanapochukuliwa kama watumishi daraja la tatu



Katika shule zetu, walimu wamekuwa nguzo kuu ya malezi, maarifa na ustawi wa jamii. Hata hivyo, kuna tabaka la walimu ambalo limekuwa likipitia maumivu ya kimya kimya, huku mchango wao ukidhihakiwa kila uchao.

Hawa si wengine bali ni walimu wa somo la Elimu ya Kiislamu (EDK) na lugha ya Kiarabu.

Nina uzoefu wa miaka mingi wa kushuhudia mtindo usio wa haki ambapo mwalimu wa Kemia, Fizikia, au Hesabu anapewa thamani kubwa, anapandishwa cheo, na kulipwa mshahara mnono, huku 'Ustadh' au 'Ustadhat' akionekana kama mtu wa ziada tu shuleni.

Huu umekuwa ubaguzi wa kimfumo na kilio cha muda mrefu ambacho sasa kinahitaji mabadiliko ya kifikra na kimfumo.

Moja ya dhana potofu inayochangia dharau hii ni mtazamo uliozoeleka kuwa walimu wa EDK ni watu walioishia mafunzo ya madrasa za mitaani pekee, wasio na weledi wa kileo. Huu ni ukweli uliopitwa na wakati. Dunia imebadilika, na sekta ya elimu imekua.

Leo hii, vyuo vikuu vingi vinavyotambulika nchini na nje ya nchi vinazalisha wasomi waliobobea katika Elimu ya Kiislamu, Sheria za Kiislamu (Shariah), na Lugha ya Kiarabu. Walimu hawa wanasoma saikolojia ya mtoto, mbinu za ufundishaji na usimamizi wa shule kama walivyo walimu wa masomo mengine ya sayansi na sanaa.

Kumchukulia mwalimu mwenye shahada ya chuo kikuu kama mtu asiye na sifa, kwa sababu tu anafundisha EDK, ni upofu wa kitaaluma na ukosefu wa haki. Mwalimu huyu anakabiliwa na mitaala ileile, anasimamiwa na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), na anapaswa kufanikisha ufaulu kama walivyo wengine. Inakuwaje basi, mtaalamu huyu anyimwe hadhi yake?

## Unyanyasaji katika shule zetu

Inasikitisha kuona kuwa unyanyasaji huu hauishii kwenye shule za kawaida tu, bali umekithiri hata ndani ya baadhi ya shule zinazomilikiwa na taasisi za Kiislamu. Shule hizi, ambazo kimsingi zilianzishwa kwa lengo la kuinua maadili na elimu ya dini, zimekuwa mstari wa mbele kuwakandamiza walimu wa EDK na Kiarabu.

Katika shule nyingi za aina hii, walimu wa EDK wanachukuliwa kama watumishi wa daraja la tatu. Maslahi yao yako chini mno ikilinganishwa na walimu wa masomo ya 'secular'.

Wakati mwalimu wa Kemia au Kiingereza anapewa mshahara mzuri, mwalimu wa EDK anaambulia posho isiyofikia hata nusu ya mwenzake, kana kwamba yeye haendi sokoni au hana familia inayomtegemea.

Heshima yao ndani ya vikao vya shule ni duni. Mara nyingi hupewa majukumu ya ziada yasiyo na malipo kama vile kuswalisha, kusimamia nidhamu, na kulea wanafunzi nyakati za usiku, kwa kisingizio cha kwamba "wanafanya kazi ya Jihadi na thawabu ziko kwa Mwenyezi Mungu."

Huku ni kutumia mgongo wa dini kunyonya nguvu kazi ya binadamu, jambo ambalo Uislamu wenyewe unalipiga vita. Jamii yetu kwa sasa inalalamika kila siku kuhusu mmomonyoko mkubwa wa maadili miongoni mwa vijana.

Matumizi ya dawa za kulevya, ushoga, wizi, ukosefu wa adabu, na ukatili vimekithiri. Swali la kujiuliza ni: nani anayeokoa kizazi hiki kisipotee kabisa? Jibu ni walimu wa malezi na dini, ambao ndio hawa 'Maustadh' wanaodharauliwa.

Mwalimu wa hesabu anafundisha mtoto jinsi ya kupata majibu ya namba, lakini mwalimu wa EDK anafundisha mtoto jinsi ya kuwa mwanadamu mwema, mwaminifu, na mwenye hofu ya Mungu. Sayansi bila maadili ni hatari; inatengeneza wasomi wezi, mafisadi, na matapeli wa kiteknolojia.

Ni makosa makubwa kuona mwalimu wa kemia ni wa thamani kuliko anayejenga utu na roho ya mtoto. Ni lazima shule zetu, viongozi wa taasisi, na wamiliki wa shule za Kiislamu wabadilike. Huu ni wakati wa kuweka mifumo ya mishahara kulingana na viwango vya elimu na sio kwa aina ya somo.

Ustadh anastahili kulipwa vizuri, kupewa ofisi nzuri, na kupewa heshima kama mtaalamu wa malezi.

Kama hatutabadilika na kuwathamini walimu hawa, tutaendelea kushuhudia vijana wanaofaulu kwa alama za 'A' katika masomo ya sayansi, lakini wakiwa na sifuri katika ubinadamu na maadili. Hapo ndipo tutakapofeli kama Umma wa Kiislamu na kama taifa kwa ujumla.

مُحرم

## HABARI TOKA KWA MAJIRANI

MAHMOUD NYAMGUMA



# Mufti Uganda atetea kuuza mali za Waislamu, ataja faida

Mufti wa Uganda, Sheikh Shaban Ramadhan Mubaje, amesema fedha zilizopatikana kutokana na mauzo ya baadhi ya mali za Baraza Kuu la Waislamu Uganda (UMSC) ziliwekezwa katika miradi inayoliingizia taasisi hiyo mapato.

Akizungumza katika makao makuu ya UMSC, Old Kampala, Mubaje amesema shamba la mifugo la Sembabule liliuzwa kwa Shilingi bilioni tano za Uganda baada ya kubainika kuwa halikuwa likizalisha mapato.

Amesema sehemu ya fedha hizo ilitumika kununua majengo ya makazi Kansanga na Namasuba, huku nyingine ikitumika kuendeleza makao makuu ya UMSC.

Mufti huyo pia amesema mapato na uwekezaji mwingine uliotokana na maamuzi hayo umewezesha UMSC kuanzisha Msikiti wa Taifa wa Gaddafi, majengo ya biashara, hospitali, chuo kikuu, kituo cha televisheni, redio na vituo vya mafunzo ya ufundi.

Ameeleza kuwa miradi hiyo sasa inasaidia kugharamia shughuli za kila mwezi za baraza na kulifanya lijitegemee kifedha.

Mubaje pia ametetea uendelezaji wa mali ya William Street kupitia mfumo wa Build-Operate-Transfer, akisema mali hiyo itarejea UMSC baada ya muda wa makubaliano.

Amesisitiza kuwa maamuzi yote yalipitishwa na vyombo halali vya uongozi wa baraza.

# 'Bakwata' ya Uganda kushirikiana kimkakati na wabunge wao Waislamu

Baraza Kuu la Waislamu Uganda (UMSC) na kundi la wabunge Waislamu wamekubaliana kuimarisha ushirikiano katika kutetea maslahi ya jamii, kukuza uchumi na kuendeleza sheria zinazowagusa Waislamu nchini humo.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika kikao cha kwanza kati ya viongozi wa UMSC na wabunge Waislamu wa Bunge la 12, kilichohudhuriwa na wabunge 29, huku wengine 15 wakituma udhuru.

Mufti wa Uganda, Sheikh Shaban Ramadhan Mubaje, amesema kikao hicho kinaanzisha ushirikiano wa kimkakati kati ya taasisi hiyo na wabunge kwa ajili ya maendeleo ya jamii ya Kiislamu.

Ameahidi pia kushirikiana kwa karibu na serikali katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo, huku akiomba viongozi wa UMSC wapewe mafunzo ya wiki moja katika Taasisi ya Taifa ya Uongozi ya Kyankwanzi.

Makamu wa Rais wa Uganda, Jessica Alupo, ameipongeza UMSC kwa kuimarisha utulivu, uvumilivu wa kidini, uraia mwema na vyanzo endelevu vya mapato.

Amehimiza wabunge Waislamu kushirikiana na UMSC kubaini vipaumbele vya sheria vinavyohusu jamii hiyo.

Alupo pia ametaja sekta ya halal kuwa fursa kubwa ya kiuchumi, akitaka Uganda iongeze uzalishaji na mauzo ya bidhaa katika nchi zenye Waislamu wengi.

MAHMOUD NYAMGUMA

# 700 watembelea Masjid Jamia, Kenya kujifunza Uislamu

Zaidi ya watu 700 wametembelea Msikiti wa Jamia jijini Nairobi katika siku yake ya saba ya wazi, iliyolenga kuwapa watu wa dini nyingine nafasi ya kujifunza kuhusu Uislamu, ibada za Waislamu na historia ya msikiti huo.


Wageni hao walitembezwa ndani ya eneo la swala, wakaelezwa historia ya msikiti na kufundishwa misingi mikuu ya imani ya Kiislamu. Pia walipata nafasi ya kuuliza maswali kuhusu mafundisho ya dini hiyo na mitazamo mbalimbali inayohusishwa na Waislamu.

Imamu wa msikiti huo, Sheikh Jamaludin Osman, amesema siku hiyo huandaliwa ili kupunguza taarifa potofu na kuwapa wageni majibu ya moja kwa moja kutoka kwa wanazuoni.

Sheikh Ibrahim Lethome alijibu maswali kuhusu tofauti kati ya Nabii Isa na Mtume Muhammad, kutenganishwa kwa wanaume na wanawake wakati wa swala, ndoa za watu wa dini tofauti na haki za wanawake katika Uislamu. Wageni pia walielezwa kuhusu vyanzo vya mafundisho ya Kiislamu, vikiwamo Qur'an, Sunna, Ijma na Qiyas.

Kila mshiriki aliondoka na kifurushi kilichokuwa na tafsiri ya Qur'an kwa Kiingereza.

Msikiti wa Jamia uliojengwa mwanzoni mwa karne ya 20 ni miongoni mwa alama muhimu za kihistoria nchini Kenya.



MAHMOUD NYAMGUMA

# Chuo Kikuu Umm Al-Qura Makka chafunza 32,000 Qur'an mtandaoni




Zaidi ya wanafunzi 32,000 kutoka nchi 90 wamenufaika na huduma za Kituo cha Qur'an Mtandaoni cha Chuo Kikuu cha Umm Al-Qura, kilichopo Makka, Saudi Arabia.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Qur'an la Kimataifa, IQNA, likinukuu Shirika la Habari la Saudi Arabia, SPA, kituo hicho kimeendelea kupanua huduma zake mwaka 2026 kwa kutumia teknolojia za kisasa kufundisha usomaji wa Qur'an kwa jamii mbalimbali za Kiislamu duniani.

Takwimu za kituo zinaonyesha kuwa jumla ya wanafunzi 32,798 walipata mafunzo kupitia mfumo huo wa mtandaoni. Mafunzo hayo yalitolewa na walimu 112 wanaume na wanawake waliobobea katika Qur'an na elimu zinazohusiana nayo.

Walimu hao walitoa jumla ya saa 4,768 za ufundishaji kwa kutumia mfumo ulioundwa kurahisisha ujifunzaji wa Qur'an kwa kuzingatia kanuni za Tajwid.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, jumla ya kurasa 35,687 zilisomwa na kusahihishwa katika kipindi hicho. Idadi hiyo inaonyesha ongezeko la mahitaji ya huduma za kituo na kuimarika kwa imani ya wanafunzi katika ubora wa programu zake.

Katika miaka ya karibuni, kituo hicho kimeendelea kupanua wigo wake wa kimataifa na kuimarisha nafasi ya Chuo Kikuu cha Umm Al-Qura katika elimu ya Qur'an kwa njia za kidijitali.

HABARI
MASHARIKI YA KATI

MAHMOUD NYAMGUMA

# Miaka 31 baadaye, Srebrenica yaendelea kuzika waathirika wa mauaji ya kimbari



Maelfu ya waombolezaji, manusura na viongozi kutoka mataifa mbalimbali wamekusanyika katika Kituo cha Kumbukumbu cha Srebrenica-Potočari kuadhimisha miaka 31 ya mauaji ya kimbari, huku mabaki ya waathirika 10 waliotambuliwa hivi karibuni yakizikwa.

Mauaji hayo yalikuwa kilele cha vita vya Bosnia vya mwaka 1992 hadi 1995, vilivyoambatana na mpango wa kuwafukuza Waislamu wa Bosnia katika maeneo yao.

Srebrenica, iliyokuwa imejaa wakimbizi, ilitangazwa na Umoja wa Mataifa kuwa "eneo salama" mwaka 1993. Hata hivyo, Julai 11, 1995, vikosi vya Waserbia wa Bosnia vilivyoongozwa na Ratko Mladić viliteka eneo hilo mbele ya walinda amani wa Umoja wa Mataifa.

Wanawake na watoto walitenganishwa na wanaume na wavulana. Katika siku zilizofuata, zaidi ya Waislamu 8,000 waliuawa, huku miili mingi ikizikwa na baadaye kuhamishwa katika makaburi mengine ili kuficha ushahidi.

Miongoni mwa waliozikwa mwaka huu ni Senad Jusić, aliyekuwa na miaka 20, na Ramo Dautović, aliyekuwa na miaka 56. Zaidi ya watu 1,000 bado hawajapatikana.

Kwa familia nyingi, mazishi hayo hayamalizi maumivu. Baadhi huchelewesha kuzika ndugu zao kwa matumaini kwamba sehemu zaidi za mabaki yao zitapatikana.

Hatidža Mehmedović alipoteza mumewe na wanawe wawili, Azmir na Almir. Alitafuta mabaki yao kwa miaka 15, lakini alipomzika Azmir, alipokea mifupa miwili pekee ya mguu. Baadaye alirejea kuishi peke yake Srebrenica, akisema alitaka kuwa karibu na watoto wake na kuthibitisha kuwa wauaji hawakufanikiwa kufuta uwepo wao.

Umoja wa Ulaya umesema kumbukumbu hiyo inapaswa kuwa wito wa kulinda ukweli, kupinga ukanushaji wa mauaji na kukabiliana na chuki kabla haijageuka kuwa janga jingine

# 'Muhammad' laongoza majina ya watoto England na Wales

Jina "Muhammad" limeendelea kuwa maarufu zaidi kwa watoto wa kiume nchini England na Wales kwa mwaka wa tatu mfululizo, kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya Uingereza (ONS).

Takwimu zilizotolewa kuhusu watoto waliozaliwa mwaka 2025 zinaonesha kuwa wavulana 5,957 walipewa jina Muhammad, kutoka 5,721 mwaka 2024.

Kutokana na tofauti za tahajia za Kiingereza, watoto wengine 1,712 waliitwa Mohammed, huku 895 wakipewa jina Mohammad. Kwa ujumla, watoto 8,564 walipewa mojawapo ya tahajia hizo tatu, zaidi ya mara mbili ya waliotajwa Noah.

Majina mengine yenye asili ya Kiislamu yaliyoingia katika orodha ya majina 100 maarufu ni Ibrahim, Yusuf na Musa, yaliyoshika nafasi ya 48, 58 na 63 mtawalia.

Kwa watoto wa kike, majina Layla, Maryam, Zara, Fatima na Anaya pia yaliingia katika orodha hiyo. Kwa mujibu wa tovuti ya 5Pillars, kuongezeka kwa matumizi ya majina hayo kunaakisi ukuaji na ushawishi wa jamii za Kiislamu nchini Uingereza.

Katika Uislamu, wazazi wengi huchagua majina ya Mitume na watu mashuhuri wa historia ya dini kwa lengo la kuwaheshimu na kutamani watoto waige tabia zao njema.

UKHTI FATIMA SS




# KCB, Mastercard wazindua kadi ya Sahl kwa huduma za Kiislamu

Benki ya KCB Kenya imeshirikiana na Mastercard kuzindua kadi ya Sahl, inayolenga kupanua huduma za malipo ya kidijitali zinazozingatia misingi ya fedha za Kiislamu.

Kwa mujibu wa TechAfricaNews, Capital FM Africa na Africa Business Communities, kadi hiyo itawawezesha wateja kusimamia matumizi, kufanya manunuzi na malipo ya kila siku kwa usalama, huku wakibaki ndani ya kanuni za Sharia.

KCB pia imezindua mtandao wa Sahl Agency Banking, utakaowawezesha wateja kuweka na kutoa fedha, kufanya malipo na kupata huduma nyingine za msingi kupitia mawakala walioidhinishwa nchini Kenya.

Mkurugenzi wa Mikakati na Ubunifu wa KCB Group, Mark Mwongela, amesema uzinduzi huo unajibu mahitaji ya wateja wanaotaka huduma za benki zinazoendana na imani na mtindo wao wa maisha.

"Kadi ya Sahl ni hatua muhimu katika kupanua upatikanaji wa huduma za benki zinazozingatia Sharia kwa kuwapa wateja njia salama, rahisi na inayoendana na maadili yao," amesema Mwongela.

Kadi hiyo inalenga pia wateja wanaotafuta huduma rafiki kwa Waislamu katika safari na maisha ya kila siku. Wamiliki wa Mastercard World Elite na Gold wataweza kupata ofa za malazi, migahawa, ununuzi na burudani kupitia mtandao wa kimataifa wa Mastercard.

Huduma nyingine ni pamoja na udhibiti wa matumizi, taarifa za miamala, huduma za usaidizi binafsi na muundo wa kadi unaoakisi maadili ya walengwa wake. Makamu wa Rais Mwandamizi wa Mastercard kwa Afrika Mashariki na Visiwa vya Bahari ya Hindi, Shehryar Ali, amesema ushirikiano huo unalenga kuimarisha ujumuishaji wa kifedha kwa kuiunganisha jamii ya benki za Kiislamu na huduma za kidijitali za kimataifa.

Uzinduzi huo unaongeza orodha ya bidhaa za kifedha zinazozingatia Sharia nchini Kenya, huku benki zikiongeza ushindani wa kuwafikia wateja ambao kwa muda mrefu hawakuhudumiwa vya kutosha na bidhaa za kawaida za benki.

## Uzbekistan kuwa kitovu cha fedha za Kiislamu Asia ya Kati?

**Uzbekistan imeongeza juhudi za kujenga sekta ya fedha za Kiislamu, ikilenga kuwa kitovu kikuu cha huduma hizo katika Asia ya Kati. Azma hiyo imejadiliwa katika Jukwaa la Tano la Benki na Fedha za Kiislamu la Jumuiya ya Nchi Huru, lililofanyika Tashkent na kuwakutanisha watunga sera, wataalamu wa fedha na viongozi wa sekta.**

**Kwa mujibu wa AnewZ, Uzbekistan tayari imepitisha sheria za awali za kuruhusu huduma za benki za Kiislamu, huku Benki Kuu ikiidhinisha taasisi za fedha ndogo kutoa bidhaa zinazofuata misingi ya Sharia. Sheria kamili ya benki za Kiislamu bado inajadiliwa.**

**Takribani asilimia 94 ya watu wa Uzbekistan ni Waislamu, hali inayoongeza mahitaji ya huduma mbadala zisizotegemea riba.**

**Washiriki wa jukwaa wamesema mageuzi hayo yanaweza kuongeza ujumuishaji wa kifedha, kuvutia uwekezaji kutoka Mashariki ya Kati na Asia ya Kusini-Mashariki, pamoja na kukuza sukuk, takaful na teknolojia za fedha za Kiislamu.**

## Takaful yatajwa fursa ya kupanua huduma za bima

**Bidhaa za takaful zinaweza kuongeza matumizi ya huduma za bima hasa katika nchi ambazo sehemu ndogo ya uchumi ndiyo inayofikiwa na bima, kwa mujibu wa chapisho jipya la Kundi la Benki ya Maendeleo ya Kiislamu.**

**Ripoti hiyo, iliyoandaliwa na Taasisi ya Benki ya Maendeleo ya Kiislamu pamoja na Shirika la Kimataifa la Kiislamu la Ufadhili wa Biashara, imesema huko Azerbaijan, takaful imewavutia watu wanaosita kutumia bima za kawaida kutokana na hofu kuhusu uhalali wake kwa misingi ya Kiislamu.**

**Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Trend, soko la bima la Azerbaijan lilikusanya ada za bima zenye thamani ya manat bilioni 1.35, sawa na dola milioni 796, mwaka 2024. Kiasi hicho kilikuwa ongezeko la asilimia 10.7 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.**

**Hata hivyo, kiwango cha matumizi ya bima kilikuwa asilimia 1.1 tu ya pato la taifa, chini ya wastani wa asilimia 6.2 katika nchi za OECD.**

## Iraq yaongoza Mashariki ya Kati idadi ya Benki

**Iraq imeongoza nchi za Kiarabu na Mashariki ya Kati kwa kuwa na taasisi 81 za benki, lakini ubora wa huduma zake bado uko chini ya matarajio.**

**Kwa mujibu wa Eco Iraq Observatory, taasisi hizo zinajumuisha benki 24 za biashara za ndani, benki 31 za Kiislamu, benki nane za serikali, benki 16 za kigeni na ofisi mbili za uwakilishi. Hata hivyo, taasisi hiyo imesema sekta hiyo bado haijakua kikamilifu katika huduma za kidijitali na za kielektroniki, huku wananchi wengi wakiendelea kuhifadhi fedha majumbani badala ya benki kutokana na ukosefu wa imani.**

**Iraq ina takribani watumiaji milioni 25 wa kadi za benki, sawa na zaidi ya asilimia 54 ya watu milioni 46.1 nchini humo.**

**Serikali imekuwa ikijaribu kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kuhamia katika malipo ya kielektroniki, lakini mpango wa kuondoa malipo ya fedha taslimu katika taasisi za umma bado haujatekelezwa kikamilifu.**

محرم

MAKALA ZA WAQF

NA IDARA YA ELIMU – AWQAF TANZANIA

# Waqf za kisasa: Kutoka magofu kwenda kiwanda cha vipaji kwa vijana na wanawake

**Kwa karne nyingi waqf imekuwa moja ya nguzo muhimu za maendeleo katika ustaarabu wa Kiislamu. Kupitia waqf zilijengwa misikiti, shule, maktaba, hospitali, visima, barabara na vituo vya huduma za jamii. Kwa lugha ya leo, waqf ulikuwa mfumo wa uwekezaji wa kijamii uliowezesha maendeleo bila kutegemea serikali pekee.**

**Hata hivyo, katika mazingira ya sasa, waqf umebaki kuhusishwa zaidi na ardhi na majengo. Kutokana na hali hiyo, vijana na wanawake wengi hawaoni nafasi yao ndani ya taasisi hii katika ekoloja ya uchumi wa Kiislamu.**

**Makala hii inachambua na kupendekeza kuwa waqf wa karne ya 21 uende mbali zaidi ya kuhifadhi mali. Waqf uwe pia chombo cha kujenga mtaji wa maarifa, ubunifu na uchumi wa kidijitali.**

## Je, Waqf wa kisasa unawezekana?

Kisheria, waqf ni kuhifadhi mali ili manufaa yake yaendelee kunufaisha jamii kwa muda mrefu. Kanuni hii haijabadilika. Kinachoweza kubadilika ni aina ya mali inayowekewa waqf na namna inavyosimamiwa.

Katika mabadiliko haya, nchi nyingi zimeanza kupanua matumizi ya Cash Waqf, ambapo fedha huwekezwa katika miradi yenye tija na mapato yake hutumika kugharamia elimu, afya, utafiti na ustawi wa jamii. Mtazamo huu umeifanya taasisi ya waqf kuendelea kuwa na mchango katika uchumi wa kisasa.

Kwa hiyo, pamoja na ardhi na majengo, tunaweza kufikiria waqf wa vifaa vya TEHAMA, maabara za ubunifu, mashine za uzalishaji, vituo vya mafunzo ya teknolojia na mifuko ya uwekezaji inayofuata misingi ya Sharia.

## Kutoka waqf wa majengo kwenda waqf wa maarifa

Katika zama hizi, taifa lenye rasilimali watu wenye ujuzi ndilo lenye ushindani mkubwa.

Kwa sababu hiyo, waqf unaweza kuwa chombo cha kuandaa wataalamu wa Artificial Intelligence (AI), Cybersecurity, Data Science, Software Engineering na teknolojia nyingine zinazoongoza uchumi wa dunia.

Badala ya kujenga jengo lisilotumika kikamilifu, waqf unaweza kujenga Waqf Coding Academy itakayotoa mafunzo kwa vijana wenye vipaji lakini wasio na uwezo wa kifedha.

Vilevile, taasisi za elimu zinaweza kupewa vifaa vya kisasa, maabara za kompyuta na walimu wenye utaalamu ili kuzalisha wahitimu wanaoweza kushindana katika soko la ajira duniani.

Mhitimu anayefanikiwa anaweza kurejesha sehemu ya mafanikio yake kwa kuchangia mfuko wa waqf ili kufadhili wanafunzi wengine. Hapo ndipo waqf unakuwa mfumo endelevu wa kujenga rasilimali watu.

## Waqf wa kidijitali na uwazi

Changamoto kubwa katika taasisi nyingi za kijamii ni suala la uwazi na uwajibikaji. Teknolojia inaweza kuwa suluhisho.

Mfumo wa kidijitali unaweza kumwezesha kila mchangiaji kuona kiasi alichochangia, mradi unaotekelezwa na taarifa za matumizi ya fedha kwa wakati unaofaa.

Aidha, teknolojia za blockchain zinaweza kutumika kuhifadhi kumbukumbu za michango na miamala kwa uwazi zaidi pale zinapofaa na kuzingatia sheria. Lengo si kufuata mtindo wa teknolojia, bali kuongeza uaminifu wa umma katika taasisi za waqf.

## Waqf na uwezeshaji wa wanawake

Wanawake ni sehemu muhimu ya maendeleo ya jamii. Kupitia Waqf Revolving Fund, vikundi vya wanawake vinaweza kupewa mitaji ya biashara bila riba kwa misingi ya Sharia. Mtaji unaporejeshwa, hutolewa kwa wanufaika wengine. Mfumo huu huongeza ajira, kipato cha familia na kujenga uchumi jumuishi.

Kadhalika, waqf unaweza kujenga hosteli salama kwa wanafunzi wanaotoka maeneo ya mbali kufuata elimu ya juu, hususan katika fani za sayansi na teknolojia. Huu ni uwekezaji wa moja kwa moja katika maendeleo ya taifa.

## Dunia tayari imeanza

Katika miaka ya hivi karibuni, Indonesia imeendelea kuendeleza mfumo wa Cash Waqf kupitia taasisi zake za fedha za Kiislamu, huku fedha zikielekezwa kwenye elimu, afya na miradi ya maendeleo.

Nchini Saudi Arabia, mageuzi ya usimamizi wa waqf yameongeza matumizi ya uwekezaji wenye tija ili kuongeza mapato yanayogharamia huduma za kijamii.

Nchini Kenya, baadhi ya taasisi za kifedha zimeendelea kuendeleza bidhaa zinazohusiana na waqf na fedha za kijamii kwa lengo la kusaidia maendeleo ya jamii.

Mifano hii inaonesha kuwa waqf unaweza kwenda sambamba na uchumi wa kisasa bila kupoteza misingi yake ya Kiislamu.

## Tanzania inapaswa kufanya nini?

Hatua ya kwanza ni taasisi zetu ni kujiandalia sera ya kitaifa ya maendeleo ya waqf inayolenga mahitaji ya kizazi cha sasa.

Hatua ya pili ni kuweka mifumo ya kidijitali ya ukusanyaji na usimamizi wa michango ili kuongeza uwazi.

Hatua ya tatu ni kuwashirikisha vijana, wanawake na wataalamu wa sheria, uchumi na teknolojia katika usimamizi wa waqf.

Hatua ya nne ni kuanzisha ushirikiano kati ya taasisi za Kiislamu, vyuo vikuu, sekta binafsi na Serikali ili kuifanya waqf kuwa sehemu ya maendeleo ya uchumi wa maarifa.

## Hitimisho

Karne zilizopita, waqf ulijenga misikiti, shule na hospitali. Karne hii tunapaswa kujenga na kuwanedeleza pia wabunifu, wahandisi, wataalamu wa akili bandia, watafiti na wajasiriamali. Waqf usibaki kuwa kumbukumbu ya historia; uwe daraja la kuelekea uchumi wa maarifa.

NA UKHTI FATIMA



# Wazo zuri la ujasiriamali linajibu matatizo halisi ya watu

**Nimeandikana sana kuhusu hili lakini bado sokamo halijaingia akilini mwa baadhi ya watu na matokeo yake biashara nyingi hufa mapema. Kuna wazo unalolipenda bila sababu na kuna wazo linajibu mahitaji ya watu.**
**Watu wengi wanaotaka kuanzisha biashara huanza kwa kujiuliza swali moja: "Ni wazo gani zuri la biashara?" Lakini wataalamu wa ujasiriamali wanasema swali bora yapi "matatizo halisi" ambayo watu wanahitaji yatatuliwe ili maisha yawe mepesi.**
**Katika ulimwengu wa biashara changa (startups), kampuni nyingi zinazofanikiwa hazikuanza na mawazo ya ajabu sana. Zilianza kwa kuona changamoto zinazowasumbua watu kila siku na kutafuta njia rahisi ya kuzitatua.**
**Ndiyo maana wataalamu wa biashara husisitiza kuwa njia bora ya kupata wazo imara la startup ni kujifunza matatizo ya watu, si kukimbilia ubunifu usio na soko.**

## Kero katika huduma

Moja ya maeneo muhimu ya kupata mawazo ya biashara ni kuangalia wateja wanaolalamika au kukerwa na huduma fulani. Watu wanapolalamika mara kwa mara kuhusu usafiri, benki, hospitali, shule au huduma za mtandaoni, mara nyingi huwa kuna nafasi ya biashara hapo.

Wataalamu wa biashara wanasema malalamiko ni ishara kuwa kuna tatizo ambalo bado halijatatuliwa vizuri. Aliyeanzisha taratibu mteja kuchukua tiketi na kusubiri aitwe namba yake akahudumiwe, hususan kwenye benki, bila shaka aliona kero ya watu kusimama foleni muda mrefu.

## Chunguza mifumo inayopitwa na wakati

Wazo jingine la biashara linaweza kupatikana kwa kuangalia kazi zinazofanyika kwa usumbufu mkubwa au kwa hatua nyingi zisizo za lazima.Katika taasisi nyingi bado kuna michakato ya kujaza makaratasi mengi, kusubiri vibali kwa muda mrefu au kufanya kazi zinazoweza kurahisishwa kwa teknolojia.

Wataalamu wa startup wanasema biashara nyingi kubwa zimefanikiwa kwa kuokoa muda, nguvu au usumbufu wa watu.

Kadri maisha yanavyozidi kuwa ya haraka, watu wanazidi kuthamini huduma zinazorahisisha maisha yao.

## Tafuta matatizo yanayogharimu pesa nyingi

Hivi karibuni nilikuwa Zanzibar ambapo ndugu yangu mmoja anafuga kuku wa mayai anasema vifaranga na hata chakula wanatoa Tanzania Bara, jambo ambalo bila shaka linawagharimu kuliko kama vingezalishwa palepale Unguja.

Wataalamu wa biashara wanaeleza kuwa startup nyingi zenye mafanikio huwa haziuzi bidhaa pekee, bali hupunguza maumivu ya kifedha kwa wateja wao.

Ikiwa biashara au watu wanapoteza pesa kutokana na tatizo fulani, mara nyingi huwa tayari kulipia suluhisho.

Kwa mfano, kampuni inayosaidia biashara kupunguza upotevu wa bidhaa, kupunguza wafanyakazi, kuimarisha usalama au kuongeza ufanisi inaweza kuwa na nafasi kubwa sokoni.

## Fuatilia tabia zinazobadilika

Mabadiliko ya tabia za watu nayo huzaa fursa mpya za biashara. Kadri watu wanavyobadilisha namna wanavyonunua, kujifunza, kufanya kazi au kutumia simu zao, mahitaji mapya huzaliwa.

Miaka michache iliyopita, watu wengi hawakuwa wakiamini sana kufanya manunuzi mtandaoni. Leo hii, biashara za kidijitali zimekua kwa kasi kubwa kutokana na mabadiliko ya tabia za watumiaji.

Wataalamu wa ujasiriamali wanasema waanzilishi makini huwa wanaangalia jamii inaelekea wapi badala ya kuangalia ilipo sasa tu. Mfano, huko tuendako wazazi wengi wa Kiislamu wanapendelea watoto wao waende shule ambayo pia inafundisha elimu ya dini (kikamilifu) ili kuepusha watoto na ratiba ngumu ya kwenda huku na huku. Hii ni fursa kwa wamiliki wa shule.

## Sikiliza malalamiko yanayojirudia

Tatizo linalojirudia mara nyingi huwa na soko tayari.

Kuna nguvu kubwa katika kusikiliza tatizo lilelile likitajwa tena na tena. Ikiwa watu wengi kutoka sehemu tofauti wanalalamikia jambo moja, huenda kuna nafasi kubwa ya biashara hapo.

Ni kwa msingi huo ndio maana wataalamu wa biashara hushauri waanzilishi kuzungumza na watu mara kwa mara badala ya kukaa ofisini wakibuni mawazo bila kuwasikiliza watumiaji halisi.

## Tumia uzoefu wako mwenyewe

Wakati mwingine wazo bora la biashara hutoka katika maisha yako mwenyewe. Changamoto uliyoipitia kazini, chuoni au katika biashara yako inaweza kuwa changamoto inayowasumbua maelfu ya watu wengine pia.

Hii huitwa "founder advantage" — mwanzilishi kuwa na uelewa mkubwa wa tatizo kwa sababu amewahi kulipitia binafsi. Biashara nyingi zilizofanikiwa zilianzishwa na watu waliotatua matatizo waliokuwa wakikutana nayo wao wenyewe kwanza.

Hata hivyo, kwa upande mwingine usichanganye uzoefu wako unaotokana na kuipitia changamoto na mapenzi tu ya kitu kutokana na hisia. Wataalamu wa startup wanaonya kuwa kosa kubwa la baadhi ya waanzilishi ni kutengeneza bidhaa wanazozipenda wao wenyewe bila kujua kama kuna watu wanaozihitaji kweli.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

# Matokeo kidato cha 6 yazalishe wabunifu

Jumatatu iliyopita, Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) lilitangaza matokeo ya mtihani wa kidato cha sita (ACSEE) uliofanyika mwezi Mei mwaka huu.

Kwa mujibu wa baraza hilo, watahiniwa 124,603 sawa na asilimia 99.56 walifaulu kwa kupata madaraja ya kwanza hadi ya tatu, hali inayoonesha kuendelea kuimarika kwa kiwango cha ufaulu nchini.

Pamoja na mafanikio hayo, matokeo ya watahiniwa 190 yalizuiwa kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo changamoto za kiafya, huku matokeo ya watahiniwa 58 yakifutwa baada ya kubainika kufanya udanganyifu.

Miongoni mwa vitendo vya udanganyifu vilivyobainika ni kuingia na maandishi ya kujikumbusha (notes) ndani ya chumba cha mtihani, kusaidiana kujibu maswali, pamoja na kutumia simu za mkononi kuingia kwenye programu za akili unde kama ChatGPT ili kujibu maswali ya mtihani.

Kwa mujibu wa kifungu cha 32 (1) cha Kanuni za Mitihani, watahiniwa hao watapewa fursa ya kurudia mtihani huo mwaka 2027. Tunawapongeza wanafunzi wote waliofanya vizuri katika mtihani huo. Vilevile, tunawapa pole wale ambao hawakufikia matarajio yao na kuwakumbusha kuwa matokeo ya mtihani si mwisho wa safari yao ya elimu na maisha, bali ni sehemu ya mchakato wa kujifunza na kujijenga kwa mafanikio ya baadaye.

Kwa wanafunzi wengi, matokeo ya mtihani wa kidato cha sita hufungua ukurasa mpya katika safari ya kuelekea elimu ya juu, taaluma na maisha ya kazi.

Hata hivyo, mafanikio ya kweli hayapaswi kupimwa kwa ufaulu wa mitihani pekee, bali pia kwa uwezo wa mhitimu kutumia maarifa aliyoyapata kuibua mawazo mapya, kubuni suluhisho na kutatua changamoto zinazoikabili jamii.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Sema: Je, wanalingana sawa wale wanaojua na wale wasiojua? Hakika wanaozingatia ni wenye akili tu." [Qur'an, 39:9]. Pia anasema: "Hakika Allah habadilishi hali ya watu mpaka wao wabadilishe yaliyo ndani ya nafsi zao." [Qur'an, 13:11].

Aya hizi zinadhihirisha kuwa elimu ni heshima na msingi wa maendeleo, lakini thamani yake huonekana pale inapogeuzwa kuwa chanzo cha ubunifu, ugunduzi na maendeleo ya jamii.

Tunapofurahia matokeo mazuri ya mtihani wa kidato cha sita, ni muhimu kutambua kuwa mafanikio hayo ni mwanzo wa safari ya kuendeleza utafiti, ubunifu na uvumbuzi utakaosaidia kuzalisha teknolojia, bidhaa na huduma zitakazochochea maendeleo ya taifa na kuboresha maisha ya wananchi.

Dunia ya leo inawathamini zaidi watu wenye uwezo wa kubuni suluhisho kuliko wale wanaotegemea ajira pekee. Hata hivyo, mafanikio hayo hayawezi kupatikana kwa juhudi za wahitimu pekee. Serikali, taasisi za elimu na sekta binafsi zina wajibu wa kuweka mazingira yanayochochea ubunifu miongoni mwa vijana.

Uwekezaji katika maabara za kisasa, vituo vya ubunifu, tafiti, teknolojia na mafunzo ya ujasiriamali ni muhimu katika kuwasaidia vijana kubadilisha mawazo yao kuwa miradi yenye tija.

Elimu yetu isiishie darasani au kwenye ufaulu wa mitihani pekee, bali iwe chachu ya kuzalisha maarifa yatakayosaidia kubuni ajira, kutatua changamoto za jamii na kuongeza ushindani wa kiuchumi.

Licha ya Tanzania kuzalisha idadi kubwa ya wahitimu wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kila mwaka, inashangaza kuona kuwa bado kuna uhaba wa wabunifu wanaoweza kubadilisha maarifa yao kuwa bidhaa, huduma au teknolojia zenye thamani ya kiuchumi.

Wahitimu wengi wameendelea kuwa watafuta ajira badala ya kuwa waajiri na wabunifu. Hata wale wanaojitahidi kubuni bidhaa au teknolojia mbalimbali mara nyingi hukabiliwa na changamoto za ukosefu wa mitaji, miundombinu na mazingira rafiki ya kukuza mawazo yao hadi kufikia hatua ya kibiashara.

Matokeo yake, taifa linaendelea kutegemea teknolojia kutoka nje licha ya kuwa na rasilimali watu wenye elimu, vipaji na uwezo mkubwa wa kufanya ubunifu wa kiwango cha kimataifa.

Hali hii inaonesha umuhimu wa kuendelea kuboresha mfumo wa elimu ili uzingatie zaidi mafunzo ya vitendo, utafiti na utatuzi wa changamoto halisi za jamii, badala ya kutegemea nadharia pekee.

Elimu bora ni ile inayomwezesha mhitimu kuwa mbunifu, mdadisi, mtafiti na mzalishaji wa maarifa yanayoweza kuleta maendeleo endelevu.

Tanzania inahitaji wahitimu wenye uwezo wa kufikiri kwa kina, kufanya tafiti, kubuni suluhisho na kushiriki kikamilifu katika kujenga uchumi unaotegemea maarifa, ubunifu na ushindani.

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 1

Na Said Rajab
0783 650 803

# Madhila yanayowakumba watoto duniani

Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu watoto na migogoro ya silaha imeonesha kuwa mwaka 2025 ulishuhudia idadi kubwa zaidi ya watoto walioathiriwa na migogoro ya kivita katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, huku matukio 38,558 ya ukiukwaji mkubwa wa haki za watoto yakiripotiwa.



# Madhila yanayowakumba watoto duniani

Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu watoto na migogoro ya silaha imeonesha kuwa mwaka 2025 ulishuhudia idadi kubwa zaidi ya watoto walioathiriwa na migogoro ya kivita katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, huku matukio 38,558 ya ukiukwaji mkubwa wa haki za watoto yakiripotiwa.

Idadi ya watoto walioathiriwa na ukiukwaji huo ilifikia 24,174, wengi wao wakiwa wasichana. Ukiukwaji huo wa haki za watoto ulijumuisha mauaji, ukatili wa kijinsia, kutumikishwa na kutekwa nyara, kunyimwa msaada wa kibinadamu, pamoja na mashambulizi dhidi ya shule na hospitali.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, ukiukwaji huu umejikita zaidi katika nchi za Palestina, Somalia, Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Myanmar. Takwimu hizi zinaonesha ukubwa wa mateso yanayowakumba watoto katika maeneo yenye migogoro na kusisitiza umuhimu wa hatua za haraka za kuimarisha ulinzi wao na kuhakikisha haki zao za msingi zinaheshimiwa.

Takwimu na ripoti za kimataifa zinaendelea kufuatilia hali halisi ya watoto katika maeneo yenye migogoro na majanga ya kibinadamu, zikifichua idadi ya kutisha ambayo bado inawakilisha sehemu ndogo tu ya majanga halisi yanayowakumba mamilioni ya watoto duniani kote.

Mamilioni ya watoto wanateseka kutokana na njaa na utapiamlo; mamilioni zaidi wamenyimwa elimu, huduma za afya, usalama na utulivu, huku idadi inayoongezeka ya watoto wakiwa wahanga wa vita na mauaji ya kimbari.

Kwa kila ripoti mpya inayotolewa, maswali yaleyale huibuka: Nani anayehusika na majanga haya? Na nani anayefaidika na kuendelea kwa hali hii?

Mikataba ya kimataifa imethibitisha haki mbalimbali za msingi za mtoto, kubwa zaidi zikiwa haki ya kuishi, haki ya maendeleo, haki ya kupata elimu, huduma za afya, matunzo, pamoja na ulinzi dhidi ya vurugu, unyanyasaji, unyonyaji na ubaguzi.

Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto, uliopitishwa mwaka 1989, ni miongoni mwa vyombo maarufu vya kimataifa vinavyothibitisha haki hizo. Pia unazilazimisha nchi zilizoridhia mkataba huo kuchukua hatua zinazohitajika kuhakikisha maslahi bora ya mtoto yanalindwa, ikiwa ni pamoja na kuwalinda wakati wa amani na vita.

Hata hivyo, nyaraka hizi muhimu za kimataifa zimebaki kuwa wino kwenye karatasi pale zinapokutana na maslahi ya mataifa makubwa.

Ukweli wa kusikitisha kuhusu hali ya watoto duniani unaonesha pengo kubwa lililopo kati ya maandishi ya kisheria na utekelezaji wake halisi, ambapo haki zilizoainishwa katika mikataba na makubaliano zimepuuzwa na kubaki kuwa kauli mbiu zisizo na utekelezaji wa kweli, haki wala uwajibikaji.

Huku rasilimali za mataifa zikiendelea kunyonywa, vita vikiendelea kuchochewa, vikwazo vikiwekwa, na serikali kandamizi na vamizi zikiungwa mkono, ripoti na takwimu za haki za binadamu zinaendelea kutolewa zikieleza madhara ya uhalifu huu, bila kushughulikia chanzo chake halisi.

Ni kana kwamba ulimwengu unatarajiwa kuzoea kuwatazama wahanga na waathirika, na kuridhika tu kwa kuwahesabu badala ya kuwaokoa. Janga halisi halipo katika ukosefu wa sheria na makubaliano, bali katika utawala wa mfumo teule wa kimataifa unaotumia sheria dhidi ya wanyonge na kuzipuuza kila zinapokinzana na maslahi ya wenye nguvu.

Kwa hakika, kile ambacho watoto wanapitia duniani kote hivi sasa si tatizo la muda mfupi katika mfumo wa dunia, bali ni matokeo ya moja kwa moja ya muundo wa kimataifa uliojengwa juu ya utawala wa kisiasa, unyonyaji wa kiuchumi na ukandamizaji wa watu kwa maslahi ya mataifa makubwa.

Tangu kuanzishwa kwake, mfumo wa kibeberu wa kimataifa umezalisha miundo ya ukoloni, uvamizi, vita na uporaji wa mali, huku wakati huo huo ukijionesha kama mlinzi wa ubinadamu na haki za binadamu.

*Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah*



DARASA LA WIKI

SEHEMU YA 1



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

# Kuwaheshimu mabinti zetu ni urithi wa Sunna ya Mtume

Katika jamii ya Kiarabu kabla ya Uislamu, watoto wa kike hawakupewa thamani waliyostahili, hali iliyosababisha baadhi ya jamii za eneo hilo kuwazika watoto wao wa kike wakiwa hai.

Katika mazingira haya magumu ya kijamii na kiutamaduni, namna Mtume Muhammad (rehema na amani za Allah zimshukie) alivyomtendea binti yake, Fatima (radhi za Allah zimshukie) ilikuwa hatua ya kimapinduzi.

Matendo yake hayakutokana tu na hisia binafsi za upendo na huruma, bali pia yalikuwa somo la wazi kwa jamii kwamba mabinti ni hazina na siyo mizigo. Hadith ifuatayo inatoa mwongozo usiopitwa na wakati kwa wazazi kuhusu kuwalea mabinti zao kwa heshima, usalama wa kihisia na imani.

Mama Aisha (radhi za Allah zimshukie) amesema: "Sijamuona yeyote anayefanana kwa karibu zaidi na Mtume wa Mwenyezi Mungu katika tabia, mwenendo na sifa kuliko binti yake Fatima. Alipomjia Mtume, alikuwa akisimama kwa ajili yake, akimshika mkono, akimbusu na kumkalisha mahali pake. Na Mtume alipomjia Fatima, naye pia alikuwa akisimama, akimshika mkono baba yake, akimbusu na kumkalisha mahali pake." [Sunan Abi Daudi, hadith namba 5217].

Hadith hii inaonesha uhusiano wa karibu kati ya Mtume na binti yake Fatima, huku pia ikitoa somo lenye nguvu la kijamii na malezi kwamba mabinti wanastahili kupendwa, kuheshimiwa na kuthaminiwa.

Kama inavyoonekana katika mfano huo, Mtume (rehema na amani za Allah zimshukie) alipoingia kwa Fatima (Allah amridhie), Fatima alisimama kwa ajili yake, akamshika mkono, akambusu na kumkalisha mahali pake.

Kwa kumheshimu binti yake hadharani, Mtume aliifundisha jamii nzima kwamba mabinti wanastahili heshima na kutambuliwa. Kitendo hicho kilikuwa kinyume na desturi za kijamii za wakati huo na kilisaidia kuainisha upya thamani ya mtoto wa kike.

Heshima inayooneshwa faraghani huimarisha uhusiano wa kifamilia, na ile inayooneshwa hadharani huthibitisha thamani ya binti mbele ya jamii.

## Upendo na usalama wa kihisia

Mtume (rehema na amani za Allah zimshukie) alionesha upendo wa dhati kwa binti yake kwa kumshika mkono, kumbusu na kumjali kwa uwazi. Upendo wa baba kwa binti yake si udhaifu, bali ni ulinzi na nguvu.

Binti anayepata upendo nyumbani hujenga hisia ya usalama, hujiamini zaidi na hujihisi kuthaminiwa. Upendo unapokosekana, binti anaweza kuutafuta kutoka kwa mtu wa kwanza anayejitokeza kumjali, bila kuzingatia kama ni salama au la.

Vilevile, upendo wa kweli nyumbani huwakinga mabinti dhidi ya hatari mbalimbali na humrahisishia mzazi jukumu la malezi yenye huruma na uwajibikaji.

## Watoto hujifunza kwa kuiga

Mtume (rehema na amani za Allah zimshukie) alipoingia kwa Fatima, alikuta naye akionesha heshima na mapenzi yale yale aliyokuwa amempa. Watoto hujifunza zaidi kwa kuona kuliko kusikia. Kuona upendo, heshima na upole hujenga maadili ya kina zaidi kuliko maneno pekee. Mtume hakudai heshima kwanza; bali aliitoa kwanza. Heshima mara nyingi hufuata mfano uliowekwa na mzazi.

Watoto wanaohisi kuthaminiwa, kulindwa na kuheshimiwa nyumbani hujibu kwa heshima inayotokana na upendo badala ya hofu. Hali hii hujenga uhusiano imara wa kifamilia unaosimama juu ya uaminifu na kuheshimiana.

## Baba humjengea binti uwezo wa kujithamini

Kwa kumkalisha Fatima mahali pake, Mtume (rehema na amani za Allah zimshukie) alionesha heshima, umuhimu na thamani yake. Uelewa wa thamani ya binti huanzia nyumbani. Heshima, uangalizi na usalama wa kihisia kutoka kwa baba hujenga kujiamini na uwezo wa kuweka mipaka sahihi katika jamii.

Hivyo basi, baba wana nafasi muhimu katika kuamua jinsi mabinti wanavyojiona na jinsi wanavyotarajia kutendewa na wengine. Mtume ni kiigizo chema kwetu, kama alivyosema Mwenyezi Mungu: "Kwa hakika mna kigezo chema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu..." [Qur'an, 33:21].

Mtume alimlea binti yake kupitia uwepo wake, huruma na matendo ya mara kwa mara, akiacha mfano wa kudumu kwa wazazi na ujumbe kwa jamii kwamba mabinti ni watukufu na wanastahili heshima.

## Somo kwa jamii

Mtume ametufundisha kwamba malezi ya mabinti yanahitaji upendo wa dhati, ulinzi, umakini na heshima. Katika jamii ambayo kihistoria watoto wa kike hawakuthaminiwa, hata kufikia hatua ya kuuawa, mafundisho ya Mtume yalikuwa ya mageuzi makubwa.



مُحرم فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Talaka kwa njia ya simu inasihi?

**Swali:** **Je, uwakilishi (wakala) wakati wa kufunga mkataba wa ndoa, kutoa ushahidi au kutamka talaka kwa njia ya simu ni sahihi?**

**Jibu:** Ikiwa itathibitika kwa yakini kabisa kuwa hiyo ni sauti ya mtu husika, basi inakubalika. Lakini ikiwa hakuna uhakika, basi haipaswi kutegemewa. Tunachukua tahadhari hii kwa sababu kuna watu walio na uhodari na uwezo wa kuiga sauti za wengine.

Hivyo, mambo ya aina hii hayawezi kutegemewa bila uhakika, kwa kuwa huenda akatokea mtu mwenye uwezo wa kubadilisha au kuiga sauti yake na kujifanya ni mtu mwingine.

Msingi wa hukumu katika suala hili si simu yenyewe, bali ni uthibitisho wa utambulisho wa anayezungumza. Ikiwa kuna yakini kwamba anayezungumza ni yule anayejitambulisha kuwa yeye, kwa njia zinazotoa uhakika, basi uwakala, ushahidi au talaka vinaweza kuthibitika.

Lakini ikiwa kuna shaka kuhusu utambulisho wake, basi mambo hayo hayapaswi kujengwa juu ya mawasiliano hayo. Hii ni kwa ajili ya kulinda haki za watu na kuzuia udanganyifu. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali:** **Tunaomba fatwa kuhusu kuuza nyumba ya waqf tuliyoachiwa na babu yetu. Tunafanya hivyo kwa sababu kizazi chetu kimeongezeka sana; nipo mimi, ndugu zangu, watoto wa ami yangu, watoto wa watoto wa ami zangu na vizazi vyao. Nyumba hiyo haitoshi tena kutuhudumia wote kwa makazi. Pamoja na hilo, kwa sasa imeamuliwa nyumba hiyo ibomolewe ili kupisha ujenzi wa barabara. Sisi kama familia tumekubaliana kugawana thamani (fedha) itakayopatikana kutokana na fidia ya nyumba hiyo. Tunauliza je, jambo hilo linajuzu?**

**Jibu:** Maadamu nyumba hiyo imewekwa Waqf uliotekelezwa na kuheshimiwa katika kipindi chote hicho, basi ni lazima iendelee kubaki katika hali yake ya kuwa waqfu.

Hairuhusiwi kuuza Waqf kwa lengo la kugawana thamani yake miongoni mwa kizazi cha aliyeweka waqfu. Badala yake, fedha zitokanazo na nyumba hiyo zinapaswa kutumika kununua mali nyingine isiyohamishika, kama vile nyumba au kiwanja, ambayo itakuwa mbadala wa Waqf huo na kusajiliwa mahakamani kuwa ni waqfu. Kisha manufaa yake yaelekezwe katika matumizi aliyoyabainisha mwanzilishi wa Waqf (waqif).

Hii ni kwa sababu kugawanya thamani ya Waqf kunasababisha kudhoofika kwa Waqf na kuuweka katika hatari ya kutoweka. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali:** **Ni ipi hukumu ya Sharia kwa mtazamo wako kuhusu kuhamisha mazulia au vifaa vya zamani vya msikiti ambavyo havitumiki tena na kuvipeleka madrasa au msikitini? Hasa ikiwa msikiti huo mwingine au madrasa hiyo ina uhitaji wa mazulia, hata kama ni ya zamani, ili yatandikwe kwa ajili ya wanaoswali msikitini au wanafunzi wa madrasa? Tunaomba ufafanuzi.**

**Jibu:** Ikiwa msikiti una samani au vifaa vya aina yoyote vilivyozidi mahitaji yake au havihitajiki tena, basi inaruhusiwa kuhamishiwa kwenye msikiti mwingine unaovihitaji.

Ikiwa hakuna msikiti unaohitaji, basi vinaweza kutumika kwa maslahi ya mafukara na masikini, au kwa mahitaji ya madrasa, na hakuna ubaya wowote katika kufanya hivyo.

Fat–wa hii inaweka msingi kwamba, mali iliyowekwa kwa ajili ya maslahi ya umma (kama msikiti) haiharibiwi wala haitelekezwi. Ikiwa haifai tena katika sehemu yake ya awali, inahamishwa kwenda sehemu nyingine yenye manufaa yanayofanana au yanayokaribiana, ili mali hiyo iendelee kutumika katika mambo ya kheri na isipotee.

Hii ni katika kutekeleza kanuni ya kifiqhi isemayo: “Kutunza mali za Waqf na kuzitumia katika manufaa yaliyokusudiwa ni wajibu kadiri inavyowezekana.” Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

مُحرم

MAKALA MAALUM

NA UKHTI FATIMA SS
0789 201 383

# Utulivu wa Makka na Madina hauna mfano



Kila mwaka, mamilioni ya mahujaji kutoka sehemu mbalimbali za dunia hutembelea Makka na Madina, miji miwili mitakatifu zaidi katika Uislamu, kwa ajili ya kutekeleza ibada za Hijja na Umra.

Mwaka huu, kuanzia Juni 14 hadi 19, takribani Waislamu milioni 1.83 kutoka kote duniani walitekeleza ibada ya Hija, wakiwemo takriban Waislamu 4,000 kutoka Tanzania.

Licha ya ugumu wa safari hiyo, mahujaji wengi humaliza ibada zao wakiwa na furaha kubwa na utulivu wa moyo. Hali hii inaweza kuelezwa kwa kiasi kikubwa na mazingira ya kiroho yanayotawala katika miji hiyo miwili, pamoja na furaha ya kufanikiwa kutekeleza mojawapo ya nguzo tano za Uislamu. Hali kama hiyo pia huonekana kwa wanaotekeleza Umra. Ingawa Umra haina taratibu nyingi kama Hijja, Waumini huimaliza wakiwa na amani na utulivu unaofanana.

Makka ni mji alikozaliwa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) na ndiko iliko Masjid al-Haram pamoja na Al-Kaaba, na ndio kitovu cha matukio mengi muhimu ya ibada ya Hija.

Mji wa Makka upo upande wa magharibi kabisa wa Saudi Arabia, karibu na pwani ya Bahari Nyekundu. Kutokana na eneo lake, una hali ya hewa ya kitropiki na joto kali ni jambo la kawaida katika sehemu kubwa ya siku.

Karibu na Makka kuna maeneo ya Muzdalifa, Mina na uwanja wa Arafa. Maeneo haya yana umuhimu mkubwa wa kidini kwa Waislamu, na pia yana nafasi ya msingi katika utekelezaji wa ibada ya Hijja.

Hali ya hewa na mazingira ya jumla ya mji huo huleta hisia za uzito na utulivu kwa wakati mmoja. Kwa mahujaji, hakuna sehemu yoyote duniani iliyo takatifu kuliko Makka, mji unaolihifadhi Nyumba ya Mwenyezi Mungu.

Ingawa Makka ina uzito mkubwa zaidi katika ibada, Madina ndio mahali ambako mahujaji wengi huenda kupata faraja na kuponya mioyo yao. Mji huo una utulivu wa pekee, na kuwepo katika eneo la Msikiti wa Mtume kunaweza kuwa uzoefu wa tiba ya moyo. Mifumo ya kunyunyiza maji katika eneo la msikiti huongeza hisia hiyo ya utulivu na faraja.

Ndani ya eneo la msikiti pia kuna kaburi la Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani). Sehemu inayozunguka eneo hilo inajulikana kama Riyadhul Jannah, yaani bustani miongoni mwa bustani za Peponi. Kwa kawaida, mahujaji hupewa muda mfupi wa takribani nusu saa kutembelea sehemu hiyo.

Kuingia katika eneo hilo kunaweza kumfanya mtu ahisi kana kwamba yupo katika kipande cha Pepo duniani. Si jambo la kushangaza kuona mahujaji wakizidiwa na hisia wanapofika katika sehemu hiyo.

Kwa mahujaji wengi, kuwepo katika eneo lote la Msikiti wa Mtume na kuswali ndani yake ni safari ya kuponya moyo na kuitakasa nafsi. Ni uzoefu ambao ni vigumu kulinganishwa na sehemu nyingine yoyote duniani.

Mbali na Msikiti wa Mtume, Madina ina maeneo mengine mengi yenye umuhimu mkubwa wa kidini. Miongoni mwake ni Mlima Uhud, Msikiti wa Qiblatain na Msikiti wa Quba. Hali ya hewa ya Madina, ambayo ni ya wastani zaidi ikilinganishwa na Makka, huongeza utulivu wa mji huo na kuufanya kuwa mahali pazuri zaidi kwa tafakuri ya kiroho. Kwa Waislamu wenye uwezo, kutembelea miji mitakatifu ya Makka na Madina kwa ajili ya kutekeleza Hijja ni wajibu wa kidini. Kwa mtazamo wa kiroho wa Muislamu mwenye kujitolea, miji hii ina nguvu kubwa ya kuleta faraja na kuponya moyo. Kwa mahujaji wengi, kuwepo katika miji hiyo huwa mojawapo ya uzoefu wenye mabadiliko makubwa zaidi katika maisha yao.

# Nini baada ya Hijja?

## Kutoka Arafa hadi maisha ya kila siku

**Katika makala iliyopita tulijadili suala la utakaso wa nafsi na kuona jinsi Hijja inavyomsaidia Muislamu kujitakasa na magonjwa ya moyo kama kiburi, husuda na chuki. Tuligundua kwamba Hijja si ibada ya mwili pekee, bali ni safari ya ndani ya moyo inayolenga kumrejesha mja katika hali ya usafi wa kiroho.**

**Miongoni mwa siku muhimu zaidi katika safari ya Hijja ni siku ya Arafa. Siku hii imepewa nafasi ya kipekee katika Uislamu na imekuwa ishara ya rehema, msamaha na ukaribu wa Mwenyezi Mungu kwa waja wake.**

**Hata hivyo, swali muhimu linabaki: Je, Arafa ni tukio la siku moja tu, au ni shule inayopaswa kuendelea katika maisha ya kila siku?**

### Arafa: Siku ya unyenyekevu mkubwa

Katika siku ya Arafa, maelfu kwa mamilioni ya mahujaji hukusanyika na kusimama katika ardhi moja, wakiwa wamevaa mavazi ya Ihram, huku wakimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu mkubwa.

Hakuna tofauti kati ya tajiri na masikini, kiongozi na raia, wala tofauti ya lugha au taifa. Wote huwa katika hali moja: hali ya unyenyekevu mbele ya Mola wao. Hii ni picha hai ya Siku ya Kiyama, ambapo wanadamu wote watakusanywa mbele ya Mwenyezi Mungu bila mali, bila vyeo na bila nguvu yoyote ya kidunia.

### Dua na rehema za siku ya Arafa

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hakuna siku ambayo Mwenyezi Mungu huwaokoa watu wengi zaidi kutokana na Moto wa Jahannam kuliko siku ya Arafa." Kauli hii inaonesha ukubwa wa rehema inayoshuka katika siku hiyo.

Katika Arafa, nyoyo hulainika, machozi hutiririka na dua hupaa mbinguni bila vizuizi. Ni siku ambayo Muislamu hujihisi akiwa karibu zaidi na Mola wake kuliko wakati mwingine wowote. Hata hivyo, rehema ya Arafa haipaswi kubaki katika siku hiyo pekee.

### Somo la Arafa: Kujitambua upya

Miongoni mwa mafunzo makubwa ya Arafa ni mwanadamu kujitambua upya. Mtu husimama mbele ya Mwenyezi Mungu akiwa hana kitu cha kujivunia isipokuwa rehema yake.

Katika hali hii, mtu hujifunza kwamba mali haina thamani bila baraka za Mwenyezi Mungu, cheo hakina maana bila uongofu wake, elimu haina thamani bila unyenyekevu, na nguvu haina maana bila msaada wake. Hili ni darasa kubwa la kuondoa kiburi ndani ya moyo wa Muislamu.

### Arafa na mabadiliko ya kweli

Mafanikio ya Arafa hayapimwi kwa wingi wa machozi yaliyomwagika pekee, bali kwa mabadiliko yanayoendelea baada ya siku hiyo. Mtu aliyefaidika na Arafa huendelea kuwa mnyenyekevu katika maisha yake ya kila siku, mchamungu hata akiwa peke yake, mwenye kuogopa dhambi hata pale zisipoonekana na watu, na mwenye kuongeza ibada zake baada ya Hijja.

Ikiwa hali ya unyenyekevu ya Arafa itaendelea kubaki ndani ya moyo wa Muislamu, basi Hijja yake itakuwa imezaa matunda halisi.

### Changamoto baada ya Arafa

Changamoto kubwa si kusimama Arafa, bali ni kuendeleza roho ya Arafa baada ya kurejea nyumbani. Katika Arafa, mazingira yote humsaidia mtu kumkumbuka Mwenyezi Mungu.

Lakini baada ya Hijja, mtu hurudi katika maisha ya kawaida, yanayojumuisha biashara zenye vishawishi, marafiki wa aina mbalimbali, mitihani ya maisha ya kila siku na mitandao ya kijamii yenye majaribu mengi.

Hapo ndipo thamani ya Arafa inapopimwa. Je, mtu ataendelea kuwa na moyo laini kama ule wa Arafa? Au moyo wake utarudi kuwa mgumu kama ulivyokuwa kabla ya Hijja?

### Kuiishi roho ya Arafa kila siku

Muislamu aliyefaidika na Hijja anatakiwa kuifanya Arafa kuwa sehemu ya maisha yake ya kila siku. Hii ina maana kwamba kila siku iwe ni siku ya kujitathmini mbele ya Mwenyezi Mungu, siku ya toba na istighfari, siku ya unyenyekevu na kumkumbuka Mola, pamoja na siku ya kujikumbusha Akhera.

Kwa namna hii, Arafa haiishii katika Kalenda ya Hijja pekee, bali inaendelea kuishi katika maisha ya Muislamu.

### Hitimisho

Arafa ni siku ya kipekee inayofundisha unyenyekevu, toba na ukaribu na Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, thamani yake ya kweli huonekana pale mafunzo yake yanapoendelea katika maisha ya kila siku baada ya Hijja.

Muislamu anayefanikiwa si yule aliyesimama Arafa pekee, bali ni yule aliyeweza kuibeba roho ya Arafa katika moyo wake hadi nyumbani kwake.

Pamoja na mafunzo yote haya, bado kuna kipengele muhimu sana katika Hijja kinachoonesha namna Muislamu anavyopaswa kuwa kioo katika jamii yake baada ya kurejea.

Je, Hujaji anapaswa kuwa mfano wa aina gani katika jamii yake? Ni wajibu gani anaoubeba baada ya kurejea kutoka katika safari hii tukufu? Na jamii inatarajia nini kutoka kwake? Hayo ndiyo tutakayoyachambua katika sehemu inayofuata ya mfululizo wa makala hizi, unaobeba kichwa: "Hujaji kama kioo cha jamii."

*Itaendelea...*

محرم

# NASAHA ZA WIKI

0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Kwanini uzinifu unaongezeka?

**Ni jambo la kawaida siku hizi kumsikia mtu akisema, "Maziwa nayapata, nifuge ng'ombe wa nini?" Kauli hiyo inaakisi mtazamo wa baadhi ya vijana ambao, wakiongozwa na tamaa za kimwili, huona hakuna sababu ya kuingia katika ndoa kwa kuwa wanaweza kukidhi haja zao za kimwili bila kubeba gharama na majukumu yanayoambatana na ndoa.**

**Kushamiri kwa tabia hii ovu hakumaanishi kuwa hukumu ya Mwenyezi Mungu imepungua thamani au imepitwa na wakati, bali ni ishara ya changamoto zinazohitaji kutafutiwa ufumbuzi kwa kurejea katika mwongozo wa Qur'an Tukufu na Sunna za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).**

**Kuna sababu mbalimbali zinazochangia kuenea kwa zinaa, ambazo jamii inapaswa kuzitambua na kuzishughulikia kwa kuzingatia mafundisho ya Uislamu.**

## *Mosi,* kukosa hofu ya Allah

Chanzo kikubwa cha maasi ni kupungua kwa uchamungu katika siri na dhahiri. Mtu mwenye imani imara hutambua kuwa Mwenyezi Mungu humwona kila wakati, hivyo hujiepusha na mambo aliyoyakataza hata pale ambapo hakuna anayemshuhudia.

Kumcha Allah humfanya Muislamu awe makini katika matendo yake na awe na uwezo wa kupambana na matamanio yanayoweza kumpeleka katika maasi.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amehimiza kuzilinda nyoyo kwa kumcha Allah wakati wote, kwani nyoyo zinapokuwa hai kwa kumtii Allah na kumuabudu hupata nguvu ya kushinda vishawishi vya nafsi.

Na uchamungu haupatikani isipokuwa kwa yule anayemjua vyema Allah na kutambua ukuu wake. Qur'an yatwambia: "Hakika wanaomuogopa Allah miongoni mwa waja wake ni wale wenye elimu." [Qur'an, 35:28].

## *Pili,* malezi duni na utandawazi

Familia ndiyo nguzo ya kwanza ya malezi. Watoto wanapokua bila kufundishwa maadili mema ya Kiislamu, maadili hayo hayawezi kuwa sehemu ya maisha yao wanapofikia utu uzima. Msingi wa tabia njema hujengwa nyumbani kabla ya mtoto kukutana na mazingira mengine ya maisha.

Katika baadhi ya familia, wazazi wamejikita zaidi katika kutafuta riziki kuliko kuwapa watoto wao malezi ya dini. Wengine huwaachia simu za mkononi, intaneti na televisheni kuwa walimu wao. Kupitia simu ya mkononi, mtoto anaweza kuanzisha mazungumzo yanayoanza kama urafiki wa kawaida lakini baadaye yakageuka kuwa uhusiano wa haramu.

Ndiyo maana Mwenyezi Mungu amekataza hata "kuikaribia" zinaa, kwa sababu Muislamu anatakiwa kujiepusha pia na mazingira na sababu zinazoweza kumfikisha kwenye dhambi hiyo.

## *Tatu,* kukosa haya na maadili

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Kuona haya (aibu) ni sehemu ya imani." [Bukhari na Muslim]. Watu wanapokosa haya, mambo yaliyokuwa yakionekana kuwa ni aibu huanza kuyaona ya kawaida. Hali hiyo huathiri mtazamo wao kuhusu mema na mabaya.

Leo hii, mavazi yasiyo ya staha, lugha chafu na uhusiano wa wazi nje ya ndoa katika baadhi ya maeneo huonekana kuwa sehemu ya maisha ya kawaida. Mabadiliko hayo ya fikra huwafanya baadhi ya watu kupuuza uzito wa dhambi ya zinaa na kuiona kana kwamba ni jambo lisilo na madhara makubwa.

## *Nne,* marafiki waovu

Marafiki anaowachagua mtu huchangia kwa kiasi kikubwa kuathiri tabia na mwenendo wake. Kijana anayezungukwa na marafiki wanaohimiza uzinzi, starehe zisizo na mipaka na matumizi ya dawa za kulevya huwa katika hatari kubwa ya kuiga tabia hizo. Kwa hiyo, kuchagua marafiki wema ni hatua muhimu katika kujilinda dhidi ya maasi.

## *Tano,* gharama za ndoa

Uislamu unahimiza kurahisisha ndoa na kuepuka kuifanya kuwa mzigo kwa wanaotaka kuoa au kuolewa. Hata hivyo, katika baadhi ya jamii, gharama kubwa za mahari, sherehe za harusi na maandalizi mengine zimeifanya ndoa kuwa ngumu kwa vijana wengi.

Kwa mfano, katika baadhi ya jamii za wafugaji, mahari ya mifugo huwa kubwa sana, ilhali katika jamii nyingine mahari hujumuisha fedha nyingi, madini au mali nyingine zenye thamani kubwa.

Katika Uislamu, mahari ni haki ya mwanamke, lakini inapaswa kuwa ya kiasi na isiyomuelemea anayetaka kuoa. Kurahisisha mahari na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima katika harusi husaidia kuhamasisha ndoa na kulinda maadili ya jamii.

## *Sita,* umasikini na tamaa ya mali

Baadhi ya watu huingia katika zinaa kwa sababu ya tamaa ya mali au kutafuta mahitaji ya kimaisha. Ingawa hali hiyo haihalalishi zinaa, inaonesha umuhimu wa jamii kupambana na umasikini, kuwasaidia wenye uhitaji na kutoa fursa za ajira ili kupunguza mazingira yanayochochea kuenea kwa maovu.

## Suluhisho la tatizo


Kupambana na zinaa kunahitaji juhudi za pamoja kutoka kwa Serikali, familia, viongozi wa dini na jamii kwa ujumla. Kwanza, elimu ya dini inapaswa kupewa nafasi kubwa katika familia, nyumba za ibada na taasisi za elimu.

Pili, wazazi wanapaswa kuwalea watoto wao katika misingi ya Qur'an na Sunna ili wawe na kinga dhidi ya maovu. Tatu, vijana wahimizwe kufunga ndoa wanapokuwa na uwezo, huku jamii ikiepuka mila na desturi zinazofanya ndoa kuwa ngumu.

**MAKALA MAALUM**

SEHEMU YA 5 YA MWISHO

Na Said Rajab
0783 650 803



# VITA MASHARIKI YA KATI:
# Pakistan ni msuluhishi halisi au kibaraka wa Marekani?

Katika makala iliyopita tulihitimisha kwa swali hili: Ni taifa gani la Kiislamu leo linalojiita ndugu wa dhati wa Palestina, Msikiti wa Al–Aqsa, Gaza, Sudan, Yemen, Afghanistan au Kashmir? Je, udugu wa kweli ni kusimama pembeni huku ndugu yako akishambuliwa, raia wake wakiuawa na miundombinu yake ikiharibiwa bila kuchukua hatua zenye uzito wa kuzuia hali hiyo? Sasa tuendelee na sehemu ya mwisho ya makala haya.

# Pakistan ni msuluhishi halisi au kibaraka wa Marekani?

Ndugu zangu katika imani, tusidanganyane. Wazo la "udugu" wa mataifa ya Waislamu duniani limebaki kuwa maneno matupu, kwa sababu ukweli ni kwamba mataifa ya kisasa ya Waislamu hayakujengwa kwa msingi wa udugu. Yalibuniwa, yakaundwa na kujengwa ili yagawanyike daima.

Baada ya Waislamu kupoteza dola yao iliyowaunganisha kwa msingi wa itikadi ya Kiislamu, waligawanywa kwa mipaka ya kijiografia, wakaendeshwa kwa misingi ya utaifa na kugawanywa kwa misingi ya ukabila.

Mazingira haya yaliwekwa na maadui wa Uislamu ili kuzuia kabisa umoja wa kweli wa Waislamu duniani.

Ndiyo maana utaona Gaza inaungua huku Waislamu wengine wakiangalia tu, Sudan inaanguka huku Waislamu wengine wakikaa kimya, Yemen inaangamizwa na mataifa mengine ya Waislamu, na Afghanistan inapigwa mabomu na jirani yake Muislamu.

Kama kweli mataifa ya Waislamu duniani yangekuwa kitu kimoja, je, tungekuwa katika hali hii leo? Ukweli ni kwamba mataifa haya hayaendeshwi kwa kuzingatia umoja wa Umma wa Kiislamu duniani. Badala yake, yanaendeshwa kwa kuzingatia maslahi ya kila taifa.

Umma unaweza kujiona kuwa kitu kimoja, lakini mfumo wa kisiasa uliopandikizwa unahakikisha kuwa mgawanyiko unaendelea kudumu. Pakistan inapaswa kuwa taifa linaloongoza, badala ya kuwa kibaraka wa mabeberu.

Ukweli ni kwamba Pakistan ina uwezo wa kuongoza Umma wa Kiislamu kutokana na nafasi yake ya kipekee ndani ya ulimwengu wa Waislamu. Ina silaha za nyuklia, jeshi lenye nguvu na uzoefu, jiografia ya kimkakati, pamoja na idadi kubwa ya watu wenye uwezo.

Hii ni misingi ya taifa linaloweza kuongoza. Swali ni: Kwanini Pakistan haichukui nafasi hiyo? Kwanini haiendeshi mambo yake kwa uhuru?

Jibu ni kwamba, licha ya kuwa na nguvu zote hizo, Pakistan haina uongozi unaojengwa juu ya itikadi.

Badala yake, uongozi wake umekuwa ukitanguliza utiifu kwa mabeberu na kubaki chini ya ushawishi wa utawala wa Marekani kwa manufaa ya muda mfupi.

Hebu fikiria, iwapo Pakistan ingeungana kwa "udugu" wa kweli na Iran pamoja na mataifa mengine ya Waislamu, yote yakiwa yameshikamana kwa kamba ya Mwenyezi Mungu, bila shaka yangeweza kuongoza dunia, kama walivyofanya Waturuki wakati wa enzi za Dola ya Ottoman.

Watu wa Pakistan, ambao ni sehemu muhimu ya Umma wa Kiislamu wanapaswa kutambua kwamba ni kupitia umoja wa kisiasa wa Umma ndipo ulimwengu wa Kiislamu utashuhudia usalama, ustawi na maendeleo kwa mara nyingine tena.

Bila hivyo, Pakistan itaendelea kuwa tarishi, kibaraka na kikaragosi katika michezo ya kisiasa inayochezwa na mataifa yenye nguvu duniani, kama Marekani.

***Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah***



NA ZAHARANI BARAKA

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

# Hivi huridhii wapate dunia, nasi tupate Akhera?

**Siku moja Umar bin Khattwab (radhi za Allah ziwe juu yake) aliingia nyumbani kwa Mtume (rehema na amani zimshukie), akamkuta amelala juu ya mkeka ambao ulikuwa umeacha alama ubavuni mwake. Chini ya kichwa chake kulikuwa na mto uliotengenezwa kwa ngozi na kujazwa nyuzi za mitende, huku pembeni kukiwa na ngozi iliyoning'inizwa. Umar alipoona hali hiyo alianza kulia. Mtume (rehema na amani zimshukie) akamuuliza: "Kwanini unalia, ewe Umar?" Umar akasema: "Ewe Mjumbe wa Allah! Kisra na Kaisari (wafalme wa Fursi na Roma) wanaishi katika starehe kubwa, ilhali wewe ni Mjumbe wa Allah?" Mtume (rehema na amani zimshukie) akamjibu: "Je, huridhii wao wapate dunia, nasi tupate Akhera?" *[Bukhari na Muslim]*.**

## Mafundisho ya tukio hili

Katika maisha ya sasa, mtazamo wa watu kuhusu maisha bora umebadilika kwa kiasi kikubwa. Wapo wanaoamini kuwa maisha ya fahari, starehe na anasa ndiyo kipimo cha mafanikio.

Wengine huona maisha mazuri kuwa ni uwezo wa kumudu kila aina ya starehe bila kuzingatia mipaka iliyowekwa na Allah. Miongoni mwao wapo wanaotamani kumiliki magari ya kifahari, nyumba kubwa, mali nyingi, mapambo ya dunia na kufurahia vyakula vya aina mbalimbali.

Mtazamo huu umewafanya wengi kuhangaika kutafuta njia zitakazowafikisha katika kiwango hicho cha maisha wanachokiona kuwa bora. Kwa baadhi ya watu, harakati hizo zimepelekea kuvuka mipaka ya maadili na kutumia njia zisizokubalika ili kufikia malengo yao.

## Mtume ni mfano bora wa kuigwa

Maisha ya Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) yamejaa matukio yenye mafunzo makubwa yanayogusa nyanja mbalimbali za maisha ya mwanadamu.

Tukio hili linaonesha maisha ya kiongozi ambaye alikuwa na uwezo wa kuishi maisha ya kifahari, lakini akachagua maisha ya kawaida na ya unyenyekevu. Maisha yake yalikuwa tofauti kabisa na mwenendo wa baadhi ya viongozi wa leo wanaoweka mkazo mkubwa katika kutafuta fahari na starehe za dunia.

Watu wengi, wakiwamo viongozi na raia wa kawaida wamekuwa wakijikita katika kulimbikiza mali na kutafuta anasa bila kujali hali za wanyonge wala kuzingatia mipaka ya Allah.

Mbali na kujiepusha na anasa za dunia, Mtume (rehema na amani zimshukie) pia aliwafundisha Masahaba zake (Allah awaridhie) kuishi kwa zuhudi na kuelekeza nyoyo zao katika kuitafuta Akhera.

Wakati mwingine alikuwa akilala juu ya tandiko jepesi lisilo na thamani kubwa na kujifunika kwa kitambaa cha kawaida. Kupitia maisha hayo, Mtume aliwafundisha watu kwamba uzuri wa maisha haupimwi kwa fahari ya macho, bali kwa kuridhika, unyenyekevu na kujiepusha na mambo yanayoweza kumweka mtu mbali na Allah.

Mtume alikuwa mfano bora wa kumcha Allah na kuwa na hofu ya kutumbukia katika mambo yanayoweza kumghadhibisha Mola wake, huku akiwahimiza pia watu wake kufanya hivyo.

Kwa hakika, maisha ya anasa yaliyopitiliza yanaweza kumpeleka mtu kwenye maasi na hatimaye kupoteza mwelekeo wa maisha. Allah anasema: "Tunapotaka kuangamiza nchi, tunawaamrisha wale waliopewa starehe kufanya uasi humo; basi hapo hukumu (adhabu) ikawa juu yao, kisha tukaiangamiza kabisa." [Qur'an, 17:16].

Pia Allah anasema: "Hatukutuma mwonyaji katika mji wowote ila wenye anasa katika mji huo walisema: Hakika sisi tunayakataa mliyotumwa nayo." [Qur'an, 34:34].

Na katika hadith iliyonukuliwa na Muslim, Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Dunia ni gereza kwa muumini na ni Pepo kwa kafiri." Aya na hadith zinaelekeza kwamba muumini hapaswi kujiachia katika starehe zinazoweza kumpeleka kwenye maasi. Badala yake, anatakiwa kujidhibiti na kuishi kwa kuzingatia mipaka aliyoiweka Allah.

## Namna ya kujiepusha na anasa

Miongoni mwa njia muhimu za kujiepusha na maisha ya anasa ni kuimarisha hofu ya Allah ndani ya moyo. Mtu anapomkumbuka Allah na kutambua kuwa maisha ya dunia ni ya muda mfupi, na kwamba atahesabiwa kwa kila alichokipata na alichokitumia, hupunguza tamaa ya kufuatilia starehe zisizo na kikomo.

Kuridhika na riziki aliyokugawia Allah na kutosheka na hali aliyokukadiria huondoa tamaa, husuda na mwelekeo wa kutafuta mali kwa njia zisizo halali.

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Hakika amefaulu aliyejisalimisha, na akapewa riziki ya kutosha, na Allah akamkinaisha kwa kile alichompa." [Muslim]. Pia Mtume amesema: "Utajiri si kuwa na mali nyingi, bali utajiri wa kweli ni utajiri wa nafsi (kutosheka)." [Sahih Muslim].

Ni muhimu kuelewa kuwa maisha ya anasa yanapozidi yanaweza kumpelekea mtu kwenye uasi na hatimaye maangamizi. Kukinai ni utajiri wa kweli na chanzo cha utulivu wa moyo. Pia ni silaha muhimu ya kupambana na tamaa, husuda na matamanio yasiyo na kikomo.

Kwa hiyo, utajiri wa kweli hauko katika wingi wa mali, bali katika moyo unaoridhika, maisha yenye baraka na kumtii Allah katika kila jambo. Muumini anatakiwa kuchagua kilicho halali hata kama ni kidogo, kuliko mali nyingi iliyopatikana kwa njia ya dhuluma, wizi, udanganyifu au utapeli.

مُحرم

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494





# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Katika toleo lililopita, tuliona jinsi Allah alivyowatia katika mitihani mbalimbali watu wa Fir-aun nchini Misri, na namna Mtume Musa alivyowaombea kwa Allah ili wapate kuzingatia na kuamini. Hata hivyo, waliendelea na msimamo wao wa kukanusha, wala hawakuamini. Hatimaye wakaangamizwa.**

### Kuzamishwa kwa Fir-aun

Miongoni mwa matukio makubwa ya ajabu na ya kweli katika historia ya mwanadamu ni tukio la kuzamishwa kwa Fir-aun pamoja na idadi kubwa ya wafuasi wake baharini. Tukio hili limeandikwa katika takriban vitabu vyote vya dini, pamoja na vile vya historia.

Lilikuwa ni matokeo ya upinzani, kiburi na ukaidi dhidi ya mafunzo waliyofikishiwa na Mtume Musa na Harun (Amani ya Allah iwashukie), yaliyoambatana na hoja, dalili na miujiza iliyothibitisha ukweli wa Utume wao.

Katika Qur'an, tukio hili limeelezewa kwa ufasaha katika sura mbalimbali, kama ifuatavyo: "Na tukamfunulia Musa ya kwamba, nenda na watu wangu wakati wa usiku (tokeni katika ardhi ya Misri lakini) bila shaka mtafuatwa. Basi Fir'aun akawatuma wakusanyao watu (waje wawazuie Wana wa Israili watapotaka kutoka) (wawaambie: hakika hawa (Wayahudi) ni kikosi kidogo tu. Nao wanatuudhi. Na sisi ni wengi (na juu ya hivi) tunawaogopa (tunapaswa kuchukuwa tahadhari).

Basi tukawatoa katika bustani na chemchem (zao wakawafuwata Wana wa Israili) na (tukawatoa) katika mahazina yao na makaazi mazuri. Ndivyo hivyo (tulivyowafanya, na tukawarithisha (yote hayo) Wana wa Israili." [Qur'an, 26:52–59].

Saa ya kuondoka ilipowadia na maandalizi yakiwa yamekamilika, Musa na watu wake walianza safari yao. Qur'an inasimulia: "Basi (watu wa Fir'aun na mwenyewe) wakawafuata (Musa na watu wake), sasa yalipoonana majeshi mawili (hayo) watu wa Musa wakasema: hakika sisi tutakamatwa. (Musa) akasema: la, kwa yakini Mola wangu yu pamoja nami, bila shaka ataniongoza (tutaokoka)." [Qur'an, 26:60–62].

### Mazingatio

Hii ni imani na yakini kubwa waliotunukiwa Mitume. Angalia hali ilivyokuwa: Wakati Fir-aun na majeshi yake walikuwa nyuma yao, Wana wa Israili walikuwa wameielekea bahari uso kwa uso huku wakimpigia Nabii Musa kelele.

Hata hivyo, Nabii Musa alikuwa na yakini kwamba kamwe Mola wake hatamtupa mkono, na alikuwa na matumaini ya dhati kuwa nusura ilikuwa mbele yake. Alisema: "Hakika Mola wangu yu pamoja nami, ataniongoza." Allahu Akbar!

Nabii Musa aliikumbuka kauli ya Allah aliyoambiwa siku ya kwanza alipotumwa kwa Fir-aun: "Msiogope, mimi niko pamoja nanyi; nasikia na naona." Hakika, muda mfupi baadaye Musa akapokea muongozo kutoka kwa Mola wake, na maajabu yakatokea.

Qur'an inaeleza: "Mara tukampelekea Musa wahyi (tukamwambia): piga bahari kwa fimbo yako, basi ikatengana na kila sehemu ikawa kama jabali kubwa. Na tukawaleta (tukawasogeza) hapo wale wengine (Fir-aun na watu wake). Na tukamuokoa Musa na waliokuwa pamoja nao wote. Kisha tukawagharikisha wengine. Hakika katika hayo kuna mazingatio, lakini wengi katika hao si wenye kuamini." [Qur,an, 26:63-67].

Muujiza huu (wa kuokolewa Wana wa Israili na kuangamizwa Fir-aun na jeshi lake) umetajwa kwa ufasaha katika surat Twaha (Qur'an, 20:77–79). Allah anasema: "Na kwa hakika tulimpelekea wahyi Musa (tukamwambia): wapeleke waja wangu usiku na ukawafanyie njia kavu baharini, usiogope kukamatwa wala usiogope lolote. Fir'aun akawafuata na majeshi yake, basi yakawafunika humo baharini yaliyowafunika. Basi Fir'aun akawapoteza watu wake na wala hakuwaongoza (kama alivyodai)."

### Fir-aun amkubali Mungu wa Musa na Harun

Wahenga walisema: "Mwisho wa ubaya ni fedheha." Ndivyo ilivyomtokea Fir-aun na kaumu yake.

Milima ya mawimbi ilipoupiga mwili wake na mauti yakamzingira, alitangaza imani kwa Mola wa haki, kama Qur'an inavyoeleza: "Na tukawavukisha Wana wa Israili bahari, basi Fir'aun na majeshi yake wakawafuata kwa dhuluma na uadui, mpaka alipofikwa na mafuriko (na umauti) akasema: nimeamini kwamba hakuna Mola apasaye kuabudiwa ila yule waliyemuamini Wana wa Israil, na mimi ni miongoni mwa waliojisalimisha!" [Qur'an, 10:90].

Imani hiyo ilikataliwa na haikumsaidia Fir-aun, kwani alijibiwa papo hapo: "Sasa (ndio unaamini) ilhali umeasi kabla, na (kwa muda mrefu) ulikuwa miongoni mwa mafisadi!" [Qur'an, 10:91].

Tukio hili lilikuwa miongoni mwa neema kubwa walizoneemeshwa Wana wa Israili. Liliwakomboa kutoka katika dhuluma, mateso na udhalili. Zaidi ya hayo, walishuhudia kwa macho yao namna adui yao alivyokuwa akinyanyaswa na mawimbi makubwa ya bahari!

*Itaendelea inshaAllah*

UONGOZI
UTAWALA

NA UKHTI FATIMA SS
0789 201 383

# Maamuzi bora hayafanywi kwa pupa



Maisha yetu yanasukumwa na maamuzi. Kuna maamuzi madogo ya kila siku, kama kutumia muda, kuchagua maneno au kupanga matumizi.

Kuna maamuzi makubwa, kama kuoa au kuolewa, kuacha kazi, kuanza biashara, kuwekeza, kuhama, kuchagua masomo au kuingia ubia. Tofauti kati ya mtu anayesonga mbele na anayejutia mara kwa mara mara nyingi haiko kwenye bahati, bali kwenye ubora wa maamuzi yake.

## Hatua kufikia uamuzi bora

Maamuzi bora hayahitaji hisia kali. Yanahitaji utulivu, taarifa na utaratibu. Mtu mwenye hekima hajiamulii kwa presha ya watu, hasira ya muda mfupi au tamaa ya matokeo ya haraka. Hujiuliza maswali sahihi kabla ya kuchukua hatua.

Hatua ya kwanza ni kufafanua uamuzi wenyewe. Watu wengi hukosea kwa sababu hawajui hasa wanaamua nini. Mtu anaweza kusema, "Nataka kubadili maisha," lakini hilo ni wazo pana sana. Swali sahihi ni: nataka kuamua nini leo? Kuacha kazi? Kuanzisha biashara? Kuendelea na masomo? Kuwekeza fedha?

Uamuzi usioeleweka huzaa matokeo yasiyoeleweka. Kabla hujaamua, andika jambo unaloamua kwa sentensi moja iliyo wazi.

## Elewa uzito wa uamuzi

Hatua ya pili ni kutofautisha maamuzi yanayoweza kurekebishwa na yasiyoweza kurekebishwa kirahisi.

Si kila uamuzi unahitaji uzito sawa. Kuchagua rangi ya nguo si sawa na kuchagua mwenzi ambaye unatumai utaishi naye hadi kifo kiwetenganishe. Kujaribu bidhaa mpya si sawa na kuuza nyumba ya familia.

Uamuzi unaoweza kurekebishwa unaweza kufanywa kwa kasi zaidi. Uamuzi wenye athari kubwa na ya muda mrefu unahitaji subira zaidi.

## Tafuta taarifa

Hatua ya tatu ni kutafuta taarifa. Watu wengi hutafuta taarifa zinazounga mkono kile walichokwishaamua moyoni. Huo ni mtego.

Kama unataka kuwekeza, usisikilize tu aliyepata faida. Sikiliza pia aliyepata hasara. Kama unataka kuingia ubia, usitazame tu ahadi; chunguza historia, tabia na uwezo wa mwenzako.

Kwa ujumla, elewa kuwa taarifa nzuri hupunguza kubahatisha.

Sambamba na kutafuta taarifa, uliza mtazamo wa wengine. Mtu mwenye akili haogopi ushauri. Lakini hachukui ushauri kutoka kwa kila mtu.

Tafuta watu wenye uzoefu, uaminifu na uwezo wa kukuambia ukweli. Usitafute mashabiki tu. Mtu anayekupinga kwa hoja anaweza kukusaidia zaidi kuliko anayekuunga mkono kwa mazoea.

## Dhana nyuma ya uamuzi

Hatua ya nne ni kutaja makadirio unayoyategemea ili uamuzi ufanye kazi. Kila uamuzi una imani fulani nyuma yake (assumptions).

Labda unadhani wateja watakuwepo. Labda unadhani mtu fulani atakusaidia. Labda unadhani kipato kitaongezeka. Yaandike makadirio hayo. Kisha jiulize: nikikosea hapa, mpango wangu bado utasimama?

## Tenganisha hisia na ukweli

Hatua ya tano ni kutenganisha hisia na ukweli. Hisia zina nafasi yake. Hofu, hasira, furaha, wivu au shauku vinaweza kukuonyesha kuna jambo ndani yako linalohitaji kusikilizwa. Lakini hisia si lazima ziwe dereva wa mwisho.

Hasira inaweza kukufanya uvunje uhusiano muhimu. Hofu inaweza kukuzuia kuchukua fursa. Furaha ya ghafla inaweza kukusukuma kutumia fedha bila mpango. Sikiliza hisia, lakini amua kwa ukweli.

## Pima matokeo na gharama zake

Hatua ya sita ni kuchora matokeo yanayowezekana. Jiulize: mambo yakienda vizuri, nini kitatokea? Yakienda kawaida, hali itakuwaje? Yakienda vibaya, nitaweza kustahimili? Tumaini ni muhimu, lakini si mkakati. Mtu mwenye maamuzi bora hujiandaa kwa mafanikio na kwa hatari. Sammbamba na hilo, hesabu gharama. Kila chaguo lina bei yake. Bei hiyo si fedha tu. Inaweza kuwa muda, afya, familia, heshima, usingizi, amani ya moyo au nafasi nyingine utakayoiacha. Ukiamua kuanza biashara, unaweza kupata uhuru, lakini pia unaweza kupoteza utulivu wa mshahara wa kila mwezi. Ukiamua kusoma zaidi, unaweza kupata maarifa, lakini utahitaji muda na gharama. Uamuzi bora huangalia faida na sadaka yake.

## Ukomo wa muda wa maamuzi

Hatua ya saba ni kuweka tarehe ya kuamua. Kuchambua ni muhimu, lakini kuchambua bila mwisho hugeuka woga.

Kuna watu hawashindwi kwa sababu wameamua vibaya, bali kwa sababu hawajaamua kabisa. Wanasubiri muda kamili, taarifa kamili na uhakika kamili. Maisha mara nyingi hayatoi ukamilifu huo. Weka muda wa mwisho, kisha amua kwa taarifa bora uliyonayo.

## Usitafute ukamilifu

Maamuzi bora hayamaanishi hutakosea. Yanamaanisha unapunguza pupa, mkumbo na majuto. Unapofafanua uamuzi, kutuliza hisia, kupima gharama, kutafuta taarifa, kuomba ushauri na kuweka muda wa kuamua, unaiheshimu kesho yako.

TUJIFUNZE

AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

# AKILI UNDE ZALISHI: Maana, matumizi na tahadhari muhimu

## Akili Unde Zalishi ni nini?

Akili Unde Zalishi ni aina ya akili unde yenye uwezo wa kutengeneza maudhui mapya baada ya kupokea maelekezo kutoka kwa mtumiaji. Maudhui hayo yanaweza kuwa maandishi, picha, sauti, video, programu za kompyuta, jedwali au michoro. Zana kama ChatGPT hutengeneza maandishi, huku nyingine zikiweza kuunda picha, muziki au video kutokana na maelezo ya maneno.

Akili Unde Zalishi haifanyi kazi kwa kufikiri kama binadamu. Huchambua kiasi kikubwa cha taarifa ilizofundishwa, hutambua mifumo iliyomo na kisha hutengeneza jibu linalofanana na mifumo hiyo. Kwa mfano, inapoombwa kuandika barua, hutabiri maneno yanayofaa kufuatana ili kuunda barua inayoeleweka. Kwa maana hiyo, ni mfumo wa hali ya juu wa kutambua na kuiga mifumo ya lugha, picha au sauti.

## Tofauti na aina nyingine za akili unde

Akili Unde Zalishi inapaswa kutofautishwa na aina nyingine za akili unde. Akili unde tabiri, kwa mfano, huchambua taarifa za zamani ili kukadiria kinachoweza kutokea baadaye. Inaweza kutumiwa kutabiri hali ya hewa, hatari ya mkopo, mahitaji ya bidhaa au uwezekano wa mgonjwa kupata tatizo fulani.

Aina nyingine ni akili unde ya utambuzi na uainishaji, inayotambua kitu kilichopo na kukiweka katika kundi linalofaa. Mfumo wa kutambua uso, barua, sauti, alama za vidole au ugonjwa katika picha ya hospitali ni mifano yake.

Pia kuna akili unde ya mapendekezo, inayopendekeza video, habari, bidhaa au muziki kutokana na tabia za mtumiaji. Mifumo mingine hufuata kanuni maalumu zilizowekwa, kama vile: "ikitokea hali fulani, chukua hatua fulani." Mifumo hiyo inaweza kuwa na akili unde, lakini si lazima iwe na uwezo wa kuzalisha maudhui mapya.

## Nguvu za akili unde zalishi

Nguvu kubwa ya Akili Unde Zalishi ni uwezo wake wa kurahisisha kazi zinazohitaji lugha, ubunifu na upangaji wa taarifa. Inaweza kusaidia kutafuta mawazo, kusahihisha sarufi, kurahisisha lugha ngumu, kufupisha nyaraka, kuandaa maswali, kutengeneza rasimu za barua na kupendekeza miundo ya makala.

Pia inaweza kusaidia kuandika au kukagua programu za kompyuta na kuunda vielelezo vya kufundishia. Kwa waandishi, walimu, watafiti na wafanyakazi wa taasisi, inaweza kuokoa muda katika kazi za awali na kurudia-rudia.

Hata hivyo, uwezo wake hutegemea sana namna inavyoelekezwa. Kadiri maelekezo yanavyokuwa wazi, ndivyo uwezekano wa kupata jibu linalofaa unavyoongezeka.

## Udhaifu wa akili unde zalishi

Uwezo wa kutoa majibu kwa haraka haupaswi kuchanganywa na kuwa na ukweli. Akili Unde Zalishi inaweza kutengeneza taarifa zisizo sahihi, marejeo yasiyokuwapo, takwimu za kubuni au nukuu ambazo hazikuwahi kutolewa.

Tatizo hili hujulikana kama "hallucination," yaani mfumo kutoa taarifa ya kubuni kwa lugha yenye kuonekana ya kuaminika. Mfumo unaweza kutoa jibu lenye mtiririko mzuri, lakini hilo halimaanishi kwamba taarifa iliyomo ni sahihi.

Aidha, mifumo ya akili unde inaweza kurudia upendeleo uliomo katika taarifa ilizofundishwa. Hali hii inaweza kuathiri namna inavyowasilisha watu, jamii, dini, lugha au tamaduni mbalimbali.

## Umuhimu wa kutoa maelekezo mazuri

Maelekezo yanayotolewa kwa Akili Unde Zalishi huitwa prompt. Prompt nzuri hueleza lengo, hadhira, muktadha, urefu, muundo na mipaka ya kazi.

Badala ya kusema, "Andika kuhusu elimu," mtumiaji anaweza kusema, "Andika utangulizi wa maneno 150 kuhusu manufaa ya elimu ya ufundi kwa vijana wa Tanzania, kwa lugha rahisi na bila kutunga takwimu."

Maelekezo mazuri husaidia mfumo kuelewa kazi inayotakiwa. Hata hivyo, prompt nzuri haiondoi ulazima wa kuhakiki matokeo.

## Wakati wa kutumia akili unde zalishi

Kabla ya kuitumia, mtu anapaswa kujiuliza kwa nini anaitumia na anatarajia kupata matokeo gani. Je, anataka kuharakisha kazi, kupata mawazo mapya, kurahisisha maelezo au kuandaa rasimu?

Pia anapaswa kujiuliza kama matokeo yanahitaji kuwa sahihi kabisa, kama ana utaalamu wa kuyahakiki na kama yuko tayari kuwajibika kwa makosa yatakayobaki.

Kwa kazi ambayo usahihi wake ni muhimu, matumizi ya Akili Unde Zalishi yanafaa tu iwapo mtumiaji ana uwezo wa kukagua kila dai na kulinganisha taarifa na vyanzo vinavyoaminika.

## Faragha, hakimiliki na uwajibikaji

Tahadhari nyingine ni faragha. Taarifa za wagonjwa, wanafunzi, wafanyakazi, wateja, watafiti au taasisi hazipaswi kuingizwa katika zana za akili unde bila kujua zinahifadhiwa na kutumiwa kwa namna gani.

Masuala ya hakimiliki na uandishi pia yanahitaji umakini. Mtumiaji hapaswi kuwasilisha kazi iliyotengenezwa na akili unde kana kwamba ni matokeo yake binafsi bila kuzingatia kanuni za taasisi, taaluma au uchapishaji.

Aidha, maudhui yanayotengenezwa yanapaswa kukaguliwa ili kubaini upendeleo, makosa ya kitamaduni na udhaifu wa lugha, hasa katika lugha zenye taarifa chache mtandaoni.

## Akili Unde zalishi kama msaidizi

Akili Unde Zalishi inafaa kutazamwa kama msaidizi, si mbadala wa akili na uwajibikaji wa binadamu. Inaweza kuharakisha kazi, kupanua mawazo na kuboresha mawasiliano.

Hata hivyo, mtumiaji ndiye anayepaswa kuhakiki ukweli, kulinda taarifa, kutambua chanzo na kuwajibika kwa matokeo ya mwisho. Teknolojia inaweza kusaidia kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, lakini haiwezi kuchukua nafasi ya busara, uzoefu na uamuzi wa binadamu.

مُحرم

# MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama



# Jinsi ya kudumisha motisha ya kufanya mazoezi

Watu wengi huanza mazoezi wakiwa na hamasa kubwa, lakini baada ya wiki chache ratiba hubadilika, uchovu huongezeka na mazoezi huachwa. Tatizo mara nyingi si ukosefu wa maarifa kuhusu faida za mazoezi. Wengi tayari wanajua kuwa mazoezi husaidia kupunguza hatari ya magonjwa ya moyo, kisukari, unene na matatizo ya afya ya akili. Changamoto kubwa ni namna ya kuyafanya kuwa sehemu ya maisha ya kawaida.

Kwa mujibu wa makala ya afya ya News-Medical, watu wanaodumu na mazoezi kwa muda mrefu mara nyingi hawasukumwi na hofu ya kuugua pekee. Huvutiwa zaidi na furaha wanayoipata, uhuru wa kuchagua aina ya mazoezi, kujiamini na msaada wa watu wanaowazunguka.

## Chagua mazoezi unayoyafurahia

Motisha ya ndani huwa na nguvu zaidi kuliko shinikizo kutoka nje. Mtu anayefanya mazoezi kwa sababu anafurahia kutembea, kuogelea, kucheza mpira au kuendesha baiskeli ana uwezekano mkubwa wa kuendelea kuliko anayefanya kwa kulazimishwa.

Hii ina maana kwamba si lazima kila mtu aende gym. Kwa baadhi, mazoezi yanaweza kuwa matembezi ya haraka, kuruka kamba, kucheza muziki, kufanya kazi za bustani au kushiriki mchezo wa timu. Kinachohitajika ni shughuli inayokufanya ujisikie vizuri na ambayo unaweza kurudia bila kuiona kama adhabu.

Hisia nzuri wakati wa mazoezi ni muhimu. Mwili unapopata uzoefu wa furaha, mafanikio na uchangamfu, akili huanza kuhusisha mazoezi na tuzo ya haraka, si mateso.

## Weka malengo yanayofikika

Malengo makubwa sana yanaweza kukatisha tamaa. Mtu anayeanza kwa lengo la kufanya mazoezi makali kila siku anaweza kuchoka haraka au kuumia.

Ni bora kuanza na hatua ndogo, kama kutembea dakika 15 mara tatu kwa wiki, kisha kuongeza muda taratibu. Mafanikio madogo hujenga kujiamini na kumfanya mtu aamini kwamba anaweza kuendelea.

Kufuatilia maendeleo pia husaidia. Unaweza kuandika muda uliotumia, umbali uliotembea au siku ulizofanya mazoezi. Hata hivyo, usijipime kwa uzito pekee. Kuboresha usingizi, nguvu, hali ya moyo na uwezo wa kupumua ni mafanikio muhimu pia.

## Tengeneza ratiba inayolingana na maisha yako

Watu wengi huacha mazoezi kwa sababu ya kazi, familia na majukumu mengine. Suluhisho si kusubiri siku ambayo utakuwa na muda mwingi, bali kupanga mazoezi katika muda unaopatikana.

Unaweza kugawa dakika 30 kuwa vipindi vitatu vya dakika 10. Unaweza pia kutembea kwenda sehemu ya karibu, kutumia ngazi badala ya lifti au kufanya mazoezi nyumbani.

Ratiba inayonyumbulika huwa rahisi kudumisha kuliko mpango mkali. Ukikosa siku moja, usione kwamba mpango wote umeharibika. Rudi katika ratiba siku inayofuata.

## Tafuta msaada wa watu wengine

Familia, marafiki na wenzako wanaweza kuongeza motisha. Kufanya mazoezi na mtu mwingine huongeza uwajibikaji na kupunguza upweke.

Kundi la kutembea, timu ya michezo au darasa la mazoezi linaweza kuleta urafiki na kufanya mazoezi yaonekane kama shughuli ya kijamii. Utafiti unaonyesha kuwa watu wanaopata moyo na msaada kutoka kwa wengine huwa na uwezekano mkubwa wa kuendelea.

Mazingira nayo yana mchango. Eneo salama, ratiba rahisi na vifaa vinavyopatikana huongeza uwezekano wa mtu kufanya mazoezi mara kwa mara.

## Sikiliza mwili wako

Watu hutofautiana katika nguvu, uwezo wa kupona na namna wanavyoitikia mazoezi. Maumivu, uchovu mkubwa na ukosefu wa maendeleo vinaweza kupunguza motisha.

Mpango wa mazoezi unapaswa kuzingatia umri, hali ya afya na uwezo wa mtu. Anayeanza anahitaji kuongeza kiwango taratibu. Kujisukuma kupita uwezo kunaweza kuleta maumivu na kumfanya mtu aache kabisa.

Kwa watu wenye magonjwa sugu au waliokaa muda mrefu bila kufanya mazoezi, ushauri wa mtaalamu wa afya unaweza kusaidia kabla ya kuanza mpango mpya.

## Tumia teknolojia kwa busara

Saa za mazoezi na programu za simu zinaweza kusaidia kufuatilia hatua, mapigo ya moyo na muda wa shughuli. Vikumbusho na taarifa za maendeleo vinaweza kuongeza uwajibikaji. Lakini teknolojia isiwe chanzo cha shinikizo. Lengo si kushindana kila siku na namba, bali kujenga tabia inayodumu.

Mwisho, motisha ya mazoezi haipaswi kutegemea hamasa ya siku moja. Hujengwa kwa kuchagua shughuli inayofurahisha, kuweka malengo madogo, kupata msaada na kurudia kwa uthabiti.

محرم

MAKALA
MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA



# Makosa wazazi yanayokuza watoto waongo

Kila mzazi anatamani kumlea mtoto mkweli. Tunataka watoto wetu wawe waaminifu, wawajibike na wasiwe na tabia ya kusema uongo. Lakini wakati mwingine, bila kujua, wazazi na walezi hutengeneza mazingira ambayo yanamfundisha mtoto kuwa kusema uongo ni salama kuliko kusema ukweli.

Saikolojia ya watoto inaonyesha kuwa watoto wengi hawaanzi kusema uongo kwa sababu ni waovu. Mara nyingi hujifunza kuwa ukweli unaambatana na hasira, adhabu au aibu, wakati uongo unaweza kuwaokoa. Ndipo uongo huanza kuwa tabia.

## Usiulize swali ambalo tayari unajua jibu

Fikiria umemwona mtoto akimpiga mdogo wake. Badala ya kusema, "Nilikuona ukimpiga kaka yako. Tuongee kilichotokea," unamuuliza, "Je, ulimpiga?"

Swali hilo linamweka mtoto kwenye mtihani. Anajua umeona kilichotokea, lakini sasa anapaswa kuchagua kati ya kusema ukweli na kuadhibiwa au kusema uongo na kutumaini ataepuka adhabu.

Njia bora ni kueleza kile ulichokiona na kuanza kutafuta suluhisho badala ya kumtega kwenye uongo.

## Pokea ukweli kwa utulivu

Mtoto akija kukueleza kuwa amevunja kikombe au amefanya kosa fulani, namna unavyoitikia ina nguvu kuliko maneno yako.

Ukipaza sauti, kumdhalilisha au kumtisha, ubongo wake hujifunza kuwa kusema ukweli ni jambo hatari. Mara nyingine ijayo atatafuta njia ya kuficha kosa.

Badala yake, mshukuru kwa kusema ukweli. Baadaye ndipo mshughulikie kosa alilofanya kwa utulivu na kwa njia ya kujenga.

## Mpe sababu ya kusema ukweli

Wakati mwingine wazazi huwaadhibu watoto sawa sawa, iwe wamekiri kosa au wamekamatwa wakidanganya. Mtoto huanza kujiuliza, "Kama adhabu ni ileile, kwa nini niseme ukweli?"

Ni muhimu mtoto aone kuwa uaminifu una thamani. Anaweza kuwajibishwa kwa kosa alilofanya, lakini ukweli wake utambuliwe na kuthaminiwa. Hilo humfundisha kuwa kusema ukweli ni uamuzi wa busara.

## Usimfanye aogope kufanya makosa

Baadhi ya wazazi huweka viwango vya ukamilifu ambavyo haviwezekani kufikiwa. Maneno kama, "Umeniangusha," "Nilitegemea mengi zaidi kutoka kwako," au "Kwa nini wewe kila mara?" yanaweza kumfanya mtoto aamini kuwa kufanya kosa kunamaanisha ameshindwa kama mtu.

Watoto wanaoogopa makosa mara nyingi huanza kuyaficha. Lakini mtoto anayejua kuwa makosa ni sehemu ya kujifunza huwa tayari kuyakiri na kujifunza kutokana nayo.

## Kuwa mfano wa uaminifu

Watoto hujifunza zaidi kwa kutazama kuliko kwa kusikiliza. Mzazi anayemwambia mtoto, "Mwambie aliyepiga simu sipo nyumbani," au "Usimwambie baba kuhusu jambo hili," anatoa somo ambalo haliwezi kufutwa kwa mahubiri kuhusu uaminifu.

Ikiwa unataka mtoto aseme ukweli, lazima nawe uwe tayari kusema ukweli hata pale unapohisi kutakuwa na usumbufu au aibu.

## Tengeneza mazingira salama ya mazungumzo

Watoto wanaosema ukweli mara nyingi ni wale wanaojua kuwa nyumbani wanaweza kusikilizwa bila kuhukumiwa haraka.

Hii haimaanishi kuwa makosa hayana matokeo. Inamaanisha kuwa mazungumzo yanatangulia hukumu. Mtoto anapopata nafasi ya kueleza kilichotokea, wazazi wanaweza kuelewa chanzo cha tatizo na kumsaidia badala ya kuishia kuadhibu tu.

## Uaminifu hujengwa kila siku

Kufundisha uaminifu si kazi ya siku moja. Hujengwa kupitia mazungumzo, mifano na namna wazazi wanavyojibu hali za kawaida za kila siku.

Mtoto anayejifunza kuwa ukweli unapokelewa kwa utulivu, makosa yanaweza kurekebishwa na wazazi wake ni watu wanaosema wanachomaanisha, hukua akiwa na msingi imara wa uadilifu.

Lengo la malezi si kupata watoto ambao hawawezi kufanya makosa. Lengo ni kulea watoto wanaothubutu kusema ukweli hata wanapokosea, wanaowajibika kwa matendo yao na wanaoamini kuwa uaminifu ni nguvu, si udhaifu. Tabia hiyo huanza kujengwa nyumbani, katika mazungumzo madogo ya kila siku, muda mrefu kabla mtoto hajafundishwa somo lolote darasani kuhusu maadili.




MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS

# Jinsi ya kubaki mtulivu unaopofanyiwa hila

**Katika maisha ya kila siku tunakutana na watu wa aina mbalimbali. Wapo wanaotutia moyo na kutusaidia kukua, lakini pia wapo wanaoweza kutumia hila za kisaikolojia (manipulations) kutushinikiza kufanya mambo tusiyoyataka.**
**Mara nyingi mbinu hizi ni za kihisia na kisaikolojia zaidi na hazihusishi kamwe na vitisho vya wazi. Hutumia hisia, maneno na mazingira kutufanya tubadili maamuzi yetu.**
**Habari njema ni kwamba saikolojia inaweza kutusaidia kutambua mbinu hizo na kujifunza namna ya kuzidhibiti bila kuingia kwenye migogoro isiyo ya lazima.**

## Dhibiti hisia, uliza maswali

Hatua ya kwanza ya kujilinda ni kujifunza kudhibiti hisia zako. Watu wanaotaka kukushawishi kwa nguvu mara nyingi hujaribu kukukasirisha, kukutisha au kukufanya ujisikie mwenye hatia.

Ukijibu kwa hasira au haraka, unawapa nafasi ya kuongoza mazungumzo. Lakini unapochukua muda kufikiri kabla ya kujibu, unarudisha udhibiti mikononi mwako.

Kama jambo linaonekana kutatanisha au linaacha maswali mengi, usikubali mara moja. Omba ufafanuzi.

Maswali kama, "Unaweza kufafanua?" au "Una maana gani hasa?" huwafanya watu waeleze hoja zao vizuri zaidi. Wakati mwingine, hoja dhaifu huonekana wazi zinapolazimika kuelezwa kwa undani.

## Kataa mashinikizo, sema hapana

Moja ya mbinu zinazotumika sana ni kuunda hali ya dharura. Unaambiwa ukichelewa kidogo utapoteza nafasi muhimu.

Ni kweli wakati mwingine maamuzi yanahitaji kufanywa haraka. Lakini mara nyingi shinikizo hutumiwa ili usipate muda wa kufikiri. Ukiomba muda wa kutafakari kabla ya kuamua, unapunguza uwezekano wa kufanya uamuzi ambao utakuja kuujutia.

Watu wengi hukubali mambo wasiyoyataka kwa sababu wanaogopa kuwakwaza wengine. Lakini uwezo wa kusema "hapana" kwa heshima ni sehemu muhimu ya afya ya kisaikolojia.

Kukataa ombi si kukataa mtu. Ni kulinda muda wako, fedha zako au mipaka yako binafsi.

## Ukimya ni nguvu, linda taarifa binafsi

Watu wengi huhisi lazima wajibu kila kauli inayotolewa. Lakini si kila jambo linahitaji majibu, na hasa majibu ya haraka.Katika mazungumzo magumu, ukimya wa muda mfupi unaweza kumpa kila mmoja nafasi ya kufikiri. Pia unaweza kuzuia kusema maneno ambayo baadaye utayajutia.

Huo ni upande mmoja wa shilingi. Upande wa pili, si kila mtu anayehitaji kujua kila kitu kuhusu maisha yako. Kadiri watu wanavyofahamu hofu zako, matatizo yako au udhaifu wako, ndivyo wanavyoweza kutumia taarifa hizo kukushinikiza.

Kuweka wazi taarifa zako binafsi si kosa. Lakini ni busara kuchagua kwa makini nani anapaswa kujua nini.

## Epuka kubishana ushinde; hisia sio lazima ziwe kweli

Lengo la mazungumzo halipaswi kuwa kumshinda mwenzako. Lengo linapaswa kuwa kuelewana.

Unapobishana ili ushinde, hisia huongezeka na mantiki hupungua. Lakini unapouliza maswali na kutafuta ukweli, unajenga nafasi ya mazungumzo yenye tija zaidi.

Wakati mwingine mtu anaweza kuzungumza kwa sauti ya juu, kwa hasira au kwa huzuni ili akufanye uamini kuwa yeye ndiye mwenye haki.

Hata hivyo, namna jambo linavyosemwa si ushahidi kwamba ni kweli. Badala ya kuzingatia sauti au hisia, jiulize ushahidi uliopo unasemaje.

## Jenga uhuru wako

Mojawapo ya kinga kubwa dhidi ya ushawishi usiofaa ni kuwa na uwezo wa kujitegemea kadiri inavyowezekana. Uhuru wa kifedha, uwezo wa kufanya maamuzi yako mwenyewe na kujiamini hupunguza nafasi ya watu kutumia mahitaji yako kukutawala.